epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Jumamosi Mei 25, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581687

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital




UKURASA WA 3

**ADAIWA KUMUUA MPENZI WAKE KWA KUMKATA KWA PANGA**



UKURASA WA 5

**ZIARA MAKONDA YAIBUA HARUFU YA UPIGAJI MAMILIONI**



UKURASA 5

**BIL. 190.7/- KUIMARISHA ELIMU SEKONDARI ZANZIBAR**

# Wizara Ardhi ni ufanisi tu

UKURASA 2



- Wananchi walamba bil 20/- kuhama hifadhini, Hifadhi ya Taifa Ruaha yamegwa kupewa wananchi
- Kibano kikali wavamizi maeneo ya wazi na vyanzo vya maji
- Migogoro 4,565 yamalizwa na kliniki tembezi za ardhi
- Mradi wa Kawe 711 uliosimama, waendelezwa, kukamilika Aprili 2026
- Yaongezwa bajeti ya bil 287.66/- kuwalipa makandarasi, watumishi
- Maombi 191 miradi ya uwekezaji yaidhinishwa, imo miradi ya tril 1/-
- Watumishi 22 wasimamishwa, saba wafukuzwa kazi kisa maadili

## TACAIDS yaanika maficho ya VVU

UKURASA 4

## Mama mzazi mbaroni madai ya utekaji mtoto kujipatia mil. 20/-

UK.2

**MICHEZO** YANGA SC KUTIKISA DAR ES SALAAM UK.24

**KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Ni ufanisi tu Wizara ya Ardhi

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

KINACHOONEKANA katika mikakati ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ni kuongeza ufanisi.

Watumishi wanaokengeuka kimaadili wanawajibishwa;kwa mwaka 2023/24 watumishi 22 wamesimamishwa kazi kupisha uchunguzi kwa tuhuma za maadili zinazowakabili, saba wamefukuzwa kazi na wawili wamepewa onyo.

Aidha, miradi iliyosimama kwa muda mrefu, ukiwamo wa Kawe 711, sasa inaendelezwa. Mradi huo umefikia asilimia 35 ukitarajiwa kukamilika Aprili, 2026 na una thamani ya Sh. bilioni 169.

Katika kushughulikia migogoro ya ardhi iliyoonekana kuwa kero kitaifa, Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imetatua migogoro 4,565 kupitia kliniki tembezi za ardhi nchi nzima.

Aidha, Wizara imeongezwa bajeti Sh. bilioni 287.66 ili kulipa madeni ya wazabuni, watumishi na makandarasi.

Huku, maombi 191 ya ardhi ya uwekezaji mkubwa, eneo la hekta 11,613 yaliidhinishwa katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Mafanikio mengine ya Wizara hiyo, ni yale yanayohusu wawekezaji wa ndani na nje, ambao thamani yake ni trilioni 1.08.

Akiwasilisha jana Bungeni Jijini Dodoma, hotuba makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Waziri Jerry Silaa, alisema kuna hitajika Sh. bilioni 178.57 kwa ajili ya kuwahamisha wananchi kutoka hifadhini na kwenye vyanzo vya maji.

Kwa mwaka wa fedha 2023/24, alisema wananchi kutoka maeneo sita nchini wamelipwa Sh. bilioni 20.1 ili kuhama kwenye maeneo hayo.

Katika hotuba yake, alisema serikali iliridhia eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 478 kutoka Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, kumegwa na kugawiwa kwa wananchi.

Alisisitiza kuwa maeneo ya wazi ni lazima yatunzwe, yalindwe na kudumishwa ili yatumike kwa shughuli za umma kama mikutano na michezo ya watoto.

Kuhusu upimaji wa viwanja na mashamba, Waziri Silaa alisema kwa mwaka wa fedha 2023/24, wizara hiyo imepima viwanja 249,340 na mashamba 7,559 yamepimwa Pamoja na na kuidhinishwa.

Mradi wa Kawe 711, alisema nao umeendelezwa baada ya kukwama kwa muda mrefu na utakamilika Aprili 2026. Kwa sasa mradi huo umefikia asilimia 35 huku, majadiliano yakiendelea ya kutekeleza Mradi wa Golden Premier Residence, kati ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na mkandarasi.

Katika maendeleo mengine, alisema nyumba 71 kati ya 100 na hoteli yenye vyumba 81 katika mradi wa Morocco Square vimeuzwa.

Ili kutekeleza mikakati ya mwaka ujao wa fedha 2024/2025, alisema vipaumbele ni kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi, kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi.

Vingine ni kuimarisha mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utunzaji kumbukumbu, upatikanaji wa taarifa za ardhi, kuhakikisha kunakuwapo na nyumba bora, ukuaji wa sekta ya miliki na kuimarisha mipaka ya kimataifa.

Ili kuimarisha mikakati hiyo, wizara hiyo imeliomba Bunge kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, (Fungu 48 na Fungu 03), jumla ya Sh.bilioni 171,372,508,000.



Rais Samia Suluhu Hassan akisaini kitabu cha maombolezo katika Ubalozi wa Jamhuri ya Kiislam ya Iran, Oysterbay jijini Dar es Salaam jana, kufuatia kifo cha Rais wa nchi hiyo, Hayati Ebrahim Raisi kilichotokana na ajali ya Helkopta nchini Iran. Kushoto ni Balozi wa Iran nchini, Hossein Alvandi Bahineh. **PICHA: IKULU**

# Mama mzazi mbaroni madai ya utekaji mtoto kujipatia mil. 20/-

**Na Romana Mallya**

MAMA mzazi wa mtoto na watuhumiwa wengine wawili wanashikiliwa na Jeshi la Polisi baada ya jaribio lao la kumficha mtoto ili kumrubuni mzazi mwenza kuwa ametekwa ili kujipatia Sh. milioni 20 kukwama.

Mtoto huyo mwenye umri wa miaka mitano, ambaye ni mwanafunzi wa Shule ya Awali Isaiah Samartan iliyoko jijini Mbeya, inadaiwa mama yake mzazi, Agnes Mwalubuli, mkazi wa Isyesye, Mbeya, ndiye aliyefanikisha azma hiyo ili kujipatia kiasi hicho cha fedha.

Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Naibu Kamishna (DCP) David Misime, alisema jana kuwa Mei 15, mwaka huu muda wa saa 11:45 jioni, baba mzazi wa mtoto huyo, Layson Mkongwi, alitoa taarifa polisi kuhusu mtoto wake kutekwa na kutakiwa kutoa Sh. milioni 20 ili kumpata.

Alisema Mkongwi, ambaye ni mfakanyakazi wa kampuni binafsi jijini Mbeya, aliliambia Jeshi la Polisi kuwa alipokea simu kutoka kwa mtu asiyefahamika na kumweleza kuwa hatampata mtoto wake hadi atakapomtumia Sh. milioni 20.

Misime alisema baada ya taarifa hiyo, Jeshi la Polisi katika uchunguzi wake lilimpata mtoto huyo akiwa salama pamoja na mtuhumiwa ambaye ni Winfred Komba (36), mkazi wa Vingunguti, Dar es Salaam, ambaye alikuwa akipiga simu ya kumtishia.

Alisema watuhumiwa wengine waliokamatwa ni mama mzazi wa mtoto huyo, Agnes, ambaye anadaiwa alipanga njama na mtuhumiwa Komba ili kujipatia kiasi hicho kutoka kwa mzazi mwenza.

"Mtuhumiwa Komba baada ya kuhojiwa, alieleza kuwa baada kupanga njama hizo, alifanikiwa kumchukuwa mtoto huyo Mei 15, 2024 na kwenda kumficha kwa rafiki yake, Hamida Njuu, anayeishi jijini Mbeya," alisema.

Misime alisema ufuatiliaji ulifanyika na Mei 24, majira ya saa 5:45 usiku, mtoto huyo alikutwa nyumbani kwa Hamida, huko Simike, Mbeya.

Alisema tukio hilo limechukuwa muda mrefu kutokana na kila ambalo walikuwa wanapanga kwa kumshirikisha mama mzazi wa mtoto huyo wakidhani ana uchungu na mtoto wake, yeye alikuwa akimfikishia taarifa mtuhumiwa mwenzake, hivyo kumfanya aendelee kujificha.

Misime alisema kutokana na tukio hilo wanawashikilia watuhumiwa hao watatu kwa ajili ya kukamilisha taratibu zingine ili kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Misime alitoa wito kwa watu wenye tabia kama hiyo wafahamu watajificha kwa muda na kukamatwa.

## Mwinyi asema kuna mazuri huduma jamii

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya mambo mengi katika kuboresha sekta mbalimbali za maendeleo ikiwamo kuleta mageuzi makubwa kwenye miundombinu ya afya, elimu na maji safi.

Amesema ujenzi wa shule na hospitali za ghorofa kwa wilaya zote za Unguja na Pemba na majimbo yote ya Zanzibar, kuenea shule za kisasa, kuimarishwa kwa miundombinu ya maji safi kwa ujenzi wa matangi ya maji na kuenezwa visima vimefanyika ili kuwaondoshea wananchi adha ya huduma za jamii sambamba na ujenzi wa barabara zenye kiwango cha lami.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Idara ya Mawasiliano, Ikulu Zanzibar, Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana kwenye Ibada ya Sala ya Ijumaa na dua maalumu aliyoandaliwa na wananchi na wazee wa vijiji vya Ukongoroni na Charawe ikiwa ni sehemu ya shukurani yao baada ya kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Ukongoroni hadi Charawe pamoja na kuipongeza serikali kwa hatua kubwa ya maendeleo iliyofikiwa kwenye kukuza huduma za jamii.

Aidha, Dk. Mwinyi aliwaahidi wananchi wa mkoa huo ujenzi wa barabara ya Tunguuu hadi Makunduchi kwa mwendelezo wa barabara hiyo iliyoishia Tunguu.

Alisema serikali imeazimia kujenga njia mbili kulia na kushoto na taa za barabarani chini ya kampuni ya Brazil. Pia aliridhia ombi la wananchi wa Chwaka kujengewa daraja kwenye barabara ya Chwaka.

Dk. Mwinyi aliwashukuru wananchi mkoa wa Kusini Unguja kwa shukurani zao na dua ya kuombea maendeleo makubwa kwa serikali yao.

Pia aliwaasa waumini na wananchi wa mkoa huo kuenedela kuliombea taifa kwa mambo makubwa mawili ikiwemo kuendelea watu kuishi kwa amani na mshikamano pamoja na kuendelea kuwaombea dua viongozi kwa kuyatekeleza yote waliyowaahidi.

Akizungumza kwenye ibada ya Sala ya Ijumaa na dua ya kuwaombea viongozi wa serikali, Khatibu wa Ibada hiyo, aliwashajihisha wananchi na waumini wa dini ya kiislamu, kuwaombea dua njema viongozi wao kwa Mwenyezi Mungu awawafikishe kwenye mambo ya heri.

Alisema Waislamu wamepewa miongozo ya dini kwenye utaratibu wao wa uongozi, ambao ni wajibu wa wanaoongozwa kuishi kwa wema na viongozi wao kwa kuwatii kwa mambo yasiyomuasi Mwenyezi Mungu, kuwaheshimu, kuwasifia kwa mazuri yao, kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

Alisema, ubora wa viongozi uko kwa wanaoongozwa kuwajali na kuwapenda viongozi wao.

## HABARI KITAIFA

# Adaiwa kumuua mpenzi wake kwa kumkatakata na panga

Na Romana Mallya

NI mauaji ya kinyama baada ya Joseph Sanura (31), maarufu kama Ngosha, kudaiwa kumkatakata kwa panga mpenzi wake, Penina Rwegoshora (28), mkazi wa Goba Center, Dar es Salaam, kwa madai ya mgogoro wa kiuhusiano.

Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, alithibitisha jana kutokea kwa tukio hilo juzi saa 1:00 asubuhi, katika baa ndogo ijulikanayo kwa jina la Penina Pub.

"Uchunguzi wa awali wa polisi umeonyesha kulikuwa na mgogoro wa kiuhusiano kati ya mtuhumiwa na marehemu kabla ya kushambuliwa na panga na mtuhumiwa. Upelelezi unakamilishwa ili mtuhumiwa afikishwe mahakamani haraka iwezekanavyo," alisema Kamanda Muliro.

Kwa mujibu wa shuhuda wa tukio hilo, ambaye hakutana jina lake liandikwe gazetini, wawili hao walikuwa na uhusiano na walikuwa wakiishi pamoja.

Alisema Penina alimuaga mpenzi wake anakwenda Tanga, ingawa inadaiwa alikwenda kuonana na mzazi mwenza wa mmoja wa watoto wake na aliporejea Dar es Salaam hakwenda kwa mpenzi wake (mtuhumiwa) badala yake alifikia eneo kulikotokea mauaji hayo.

"(Mtuhumiwa) alipoona mpenzi wake hapokei simu, akaenda kwenye Pub na kumkuta hapo ndipo akamkata mapanga na baada ya kumuua akaondoka na panga lake kujisalimisha polisi," alidai shuhuda huyo mkazi wa Goba.



# Majeruhi mlipuko kiwanda cha Mtibwa wafariki dunia

Na Waandishi Wetu

MAJERUHI wawili wa tukio la mlipuko uliotokea katika chumba maalum cha uendeshaji wa mitambo kwenye kiwanda cha Sukari cha Mtibwa, mkoani Morogoro, wamefariki dunia katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamin Mkapa (BMH), Dodoma na kufanya idadi ya waliokufa kufikia 13.

Tukio la mlipuko huo lilitokea juzi katika kiwanda hicho na kusababisha vifo vya watu 11 papo hapo na majeruhi hao ambao ni Geogre Malekela (27) na Michael Kadudu (29).

Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya Dharura wa BMH, Dk. George Dilunga, alithibitisha kutokea kwa vifo hivyo ambapo mgonjwa alifariki juzi na mwingine alfajiri jana akiwa Chumba cha Wagonjwa Mahututi (ICU).

Dk. Dilunga alisema walifikishwa hospitalini hapo kutokana na majeraha waliyopata baada ya kutokea kwa mlipuko huo.

"Juhudi za madaktari kuokoa maisha ya majeruhi hawa hazikufanikiwa kutokana na changamoto walizopata katika ajali hiyo. Madaktari wamejitahidi kadri ya uwezo wao kuokoa maisha ya watu hawa, lakini kwa bahati mbaya wote wawili wamepoteza maisha kwa nyakati tofauti," alisema Dk. Dilunga.

Meneja wa Kitengo cha Umeme na Vifaa wa Kiwanda hicho, Juma Palamba, akizungumza na waandishi wa habari muda mfupi baada ya tukio hilo alitaja waliofariki dunia ni raia watatu wa kigeni kutoka nchi za Brazil, Kenya na India.

Aidha, katika tukio hilo, watanzania wawili walijeruhiwa wakati wakifanya majaribio ya mtambo wa mvuke uliokuwa umeboreshwa kwa kuongezewa nguvu ya uendeshaji.

**IMEANDALIWA na Paul Mabeja na Renatha Msungu, (DODOMA)**


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala.
   Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

RIPOTI MPYA WHO

# TACAIDS yaanika maficho ya VVU

Na Romana Mallya

SIKU tatu baada ya Shirika la Afya Duniani (WHO) kutoa ripoti ya hali ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) na magonjwa ya zinaa, Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) imeizungumzia ripoti hiyo, ikitaja ugumu inaokabiliana nao katika kuzuia maambukizi mapya ya VVU nchini.

Mei 21, mwaka huu, WHO ilitoa ripoti ikionyesha UKIMWI bado haujapungua duniani, huku zaidi ya watu milioni moja wakiambukizwa kila mwaka magonjwa ya zinaa, yakiwamo kaswende na kisonono.

Jana, katika mazungumzo mahsusi na mwandishi wa habari hii juu ya ripoti hiyo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji TACAIDS, Dk. Jerome Kamwela, aliorodhesha mambo manne yanayokwamisha jitihada za kukabiliana na janga hilo nchini.

Alitaja vikwazo hivyo ni hali ngumu ya uchumi kwa wanawake inayowasukuma kurubunika kirahisi na kuingia kwenye ngono zembe na usiri miongoni mwa wenza kushindwa kuwaeleza wenzao hali zao kiafya hata baada ya kutambua wana maambukizi.

Dk. Kamwela alitaja kikwazo cha tatu ni unyanyapaa katika jamii dhidi ya watu wanaoishi na VVU (WAVIU), unaochagiza hofu ya kupima kutambua hali ya kiafya.

Kikwazo cha nne, kwa mujibu wa Dk. Kamwela, ni nchi kuendelea kutegemea wafadhili kutoka nje, jambo analolitafsiri ni hatari na kushauri serikali kuwekeza fedha za ndani kuwanusuru wananchi dhidi ya janga hilo.

**MAAMBUKIZI YAPUNGUA**

Hata hivyo, Dk. Kamwela alisisitiza kuwa maambukizi mapya yameendelea kupungua mfululizo kwa zaidi ya asilimia 50.

"Mwaka 2010 tulikuwa na karibu watu 110,000 wanaopata maambukizi kila mwaka. Sasa hivi tumesema tuko kwenye 60,000. Hata vifo vitokanavyo na UKIMWI vimepungua kwa zaidi ya theluthi mbili.

"Unyanyapaa miaka 10 iliyopita tulikuwa tuna asilimia 25, sasa hivi tuna asilimia tano. Tunaendelea kupata faida. Pamoja na mafanikio haya, kuna changamoto za makundi," alisema.

Dk. Kamwela alisema kwenye malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 yako malengo matatu, mawili wanayafikia na moja lenye changamoto ni kutambua watu wanaoishi na VVU.

"Kwenye mafanikio, mengine tuliyo nayo ni kuendelea kupunguza maambukizi mapya na kuendelea kupunguza vifo vinavyotokana na UKIMWI na kuendelea kupunguza unyanyapaa.



Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Jerome Kamwela

"Changamoto, maambukizi yameendelea kutokea na kuna shida kwenye makundi, moja ni kundi la vijana wanaochangia theluthi moja ya maambukizi mapya, walioko shuleni, vyuoni na mitaani. Kundi ambalo tunafikiri linahitaji kufikiwa kwa karibu.

"Tuna makundi maalumu, watu ambao wanaofanya kwa mfano, biashara za ngono, wanaotumia dawa za kulevya, wanaofanya kazi za kuhamahama mfano, madereva wa masafa marefu, wavuvi, wanaoishi kwenye visiwa. Haya ni makundi ambayo yanafanya ile kasi ya kupunguza maambukizi mapya iwe ngumu, alisema.

Pia alisema hata kupata huduma za tiba ili wafubaze virusi ni ngumu kwa sababu ni watu ambao wanatoka sehemu moja kwenda nyingine.

"Tunajaribu kuzifanya programu zetu kufikia makundi haya kulingana na utofauti wao. Pia kuna watu wanaofanya kazi kwenye migodi midogo ya madini isiyo rasmi. Yako maeneo hayo kweli tunaona tunahitaji kufanyia kazi," alisema,

Alisema hayo ndiyo makundi makubwa muhimu ambayo hawajayafikia na wanafikiri kwa kipindi kilichobaki cha sasa hadi ifikapo 2030 kwa kutumia nguvu zao na serikali na sekta binafsi na wadau wa maendeleo, miradi yao inayowalenga inaweza kuonesha mafanikio chanya.

**HALI KWENYE FAMILIA**

Dk. Kamwela alisema jambo kubwa wanaliona katika familia ni unyanyapaa, ambapo bado suala la uwazi juu ya masuala ya UKIMWI ni tatizo.

Alisema kuna familia ambazo mwenza mmoja anaishi na maambukizi na mwezake asijue na ziko ambazo mtoto anaweza kupata maambukizi familia ikaona ni shida isiwaambie watu ili wamsaidie na kumlinda.

"Kuna kesi za unyanyapaa, unyanyasaji wa kijinsia. Watoto wanabakwa na ndugu wa familia na hayo mambo yanazungumzika tu ndani ya familia hayachukuliwi hatua za kisheria.

"Haya yote ndiyo tunaona kwenye familia zetu tunatakiwa kuongeza nguvu. Kuelimisha familia zetu ili waone kuna mambo yakitokea waone mtu akipata maambukizi ni kama ugonjwa mwingine, asaidiwe kupelekwa hospitalini akapimwe, apewe tiba na akirudi asinyanyapaliwe asaidiwe.

**MAENEO YANAYOWEKEWA NGUVU**

"Vinapotokea vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia au vingine vyenye matukio hasi ambavyo ni sehemu ya mila potofu kama kukeketa watoto, ndoa za utotoni.

"Ninafikiri ni miongoni mwa maeneo ambayo kwa sasa tunayawekea nguvu zaidi, katika ngazi ya familia kwa sababu yanatokea ndani ya familia ambapo si rahisi kuyajua na kuchukua hatua stahiki," alisema.

Katika mpango ho, alisema wanashirikiana na wadau wao wa maendeleo kuhakikisha wanachangia utaalam, rasilimali za kutekeleza afua, sekta ya umma ikiwamo Wizara ya Afya kuhakikisha huduma zinafika kila mahali ili jamii izifikie.

Pia alisema wanashirikiana na viongozi wa dini kuhakikisha kwenye mihadhara yao wanatoa elimu ya kupunguza unyanyapaa, watu wawe jasiri wanapojikuta na maambukizi ili wakapate huduma stahiki.

Kadhalika, alisema katika sekta usafirishaji barabara kutoka Dar es Salaam- Tunduma njiani wameweka vituo kwa ajili ya kutoa huduma kwa waendesha magari masafara marefu zaidi wanakolala ili wapate elimu na huduma.

Pia alisema wanashirikiana na sekta binafsi kwa kuwa ndiyo inaajiri sana, kuhakikisha huduma za kinga zinakuwapo mahali pa kazi na pia, kuwalipia watumishi wao wanaohitaji matibabu na huduma zingine za afya.

"Hatusemi hatujakwama, kama nilivyokuonesha matokeo tuliyopata na mafanikio yetu tunaendelea bado kuhakikisha nguvu za wadau wote tunazitekeleza na kufikia malengo tuliyojiwekea.

Hata hivyo, alisema changamoto ni kwamba mahitaji ya huduma kwa nchi ni makubwa kuliko uwezo na suala la rasilimali fedha, ambayo ni kazi ambayo tume inashirikiana na wadau wa maendeleo na serikali kuhakikisha afua za UKIMWI zinafadhiliwa kwa kiwango kinacholeta tija.

**MAKUNDI HATARISHI**

Dk. Kamwela alisema vijana ni nguvu kazi ya nchi, lakini wana madhaifu na wengi hawajajenga nguvu za kiuchumi, tegemezi, wapo katika ngazi mbalimbali za elimu.

Alisema kundi hilo kama halipati elimu ya kutosha ya kujikinga, watu wazima wenye nguvu za kiuchumi ni rahisi kuwarubuni kwenye ngono, ndio maana wana mchango wa theluthi moja ya maambukizi mapya.

"Kina mama nao ni vivyo hivyo, mila na desturi zetu zinafanya wasiwe na nguvu ya uchumi, wasiwe na uwezo wakutoa uamuzi yanayohusu hata saa nyingine yanayohusu afya zao.

"Inabidi wasubiri au waombe ruksa kwa wenza wao ambao ni wanaume. Pia takwimu zinaonesha mzigo mkubwa wa mama upo kwa kina mama na wasichana, ndio maana serikali inaangalia sana masuala ya unyanyasaji wa kijinsia na mila potofu. Hili ni eneo ambalo sisi tunasema linahitaji kuangaliwa upya ili kuwa na miradi mikubwa," anashauri.

Alisema kuna mradi wa wasichana malehe ambao umesaidia vijana wa kike na wanawake vijana ambao hawana nguvu za kiuchumi na wapo katika hatari ya kupata maambukizi kuweza kupata elimu.

Hata hivyo, alisema kama mtaalam yote hayo wakitaka kuyapunguza kwa haraka ni kuwezeka kuzuia maambukizi kundi la hilo.

Pili, alisema kuondoa vikwazo vinavyofanya kundi hilo lishindwe kupata huduma na kujikimu kiuchumi na kutegemea kufanya biashara hatari za kuwaweka kupata maambukizi.

Alitaja jambo la tatu ni kushawishi sekta binafsi kusaidia kuwekeza katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

"Mapambano hayawezi kuwa endelevu kama wataendelea kutegemea ufadhili kutoka nje. Sasa hivi kama watanzania tuchukue jukumu la kuwekeza katika kuwakinga raia wetu," alishauri.

Alitolea mfano sehemu za starehe kuwa kundi kubwa linalotoa huduma ni vijana wa kike na vijana wanawake, hivyo lazima wawakinge lisitumbukia katika ngono zembe.

**EAC NA SADC**

Alisema asilimia 90 ya mzigo wa UKIMWI duniani upo kwenye nchi za Mashariki na Kusini mwa Bara la Afrika.

"Tunafikiri Tanzania tuko vizuri tukijilinganisha na wenzetu, hali yetu ni nzuri na kitakwimu tunafikiri tutafikia malengo na tulishatajwa miaka miwili iliyopita tulikuwa kati ya nchi tano za Afrika zilizotimiza malengo," alisema.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama (kulia), akimsikiliza Mkurugenzi wa kampuni ya Global Survey, David Msungu (kushoto), alipotembelea maonyesho yaliyoandaliwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ziara ya Makonda yaibua harufu ya upigaji Fedha

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

ZIARA ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, katika wilaya sita za mkoa huo kwa ajili ya kukagua maendeleo na kutatua kero za wananchi, imeibua madudu ikiwamo viashiria vya upigaji fedha katika miradi.

Kutokana na kuwapo kwa madudu hayo, ameagiza kuundwa timu ya kuchunguza miradi yote iliyoko wilayani Longido, ikiwamo Shule ya Sekondari ya Wasichana Samia.

Makonda alitoa maagizo hayo juzi jioni wakati akizungumza na wananchi Namanga, mpakani mwa Tanzania na Kenya akiwa kwenye ziara yake ya wilaya sita za mkoa wa Arusha kukagua miradi na kutatua kero za wananchi.

Makonda alisema amejulishwa kupima udongo kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo kumegharimu Sh. milioni 10, deni la maji Sh. milioni tano na kuingiza umeme zimetumika Sh milioni 1.6.

"Tumepewa hela na Rais Samia Suluhu Hassan, tunataka kupata matumizi yake, yaani kupima udongo tu mnatumia Sh. milioni 10 katika ujenzi wa shule na ushuru wa gari la halmashauri walikuwa wanalipia kwa maelekezo ya mkurugenzi Sh. milioni tatu. Lilikuwa linafanya kazi gani, yaani gari lilitumika kusombea mchanga diwani naomba usogee karibu," alisema Makonda.

Makonda alimtaka mkuu anayesimamia ujenzi wa shule hiyo, Daniel Temu, kueleza nyongeza ya fedha ambapo alisema kupima ubora wa zege Sh. 400,000 na gharama za LUKU Sh. milioni mbili

"Hiyo Sh, milioni mbili kwa muda gani? Kwa hiyo ujenzi ulivyokamilika mkaweka LUKU. Ujenzi ulianza Septemba 30, mwaka jana na kutoka Septemba hadi Machi, mwaka huu, ni miezi sita kwa hiyo mmetumia umeme wa Sh, milioni 2.5. Je, kuna watu wanaishi pale shuleni?" alihoji Makonda.

Mkuu huyo wa mkoa alimwita Diwani wa Orbomba ambaye alisema lori la halmashauri linawadai Sh, milioni 30 na fedha iliyolipwa ni Sh milioni tatu, hivyo bado wanadai Sh milioni 27.

Alisema ujenzi wa shule hiyo wananchi hawajashirikishwa hata yeye na mwenyekiti hawakuwa wanajua chochote.

"Hata mafundi wamepatikana nje ya utaratibu. Mafundi wote wa Longido hakuna hata mmoja aliyepata kazi. Sisi hawatupi taarifa hata nikidai taarifa napewa nusu nusu," alisema diwani huyo.

Baada ya maelezo hayo, Makonda alisema: "Sasa mwalimu, diwani amesema gari la halmshauri lilitakiwa kulipwa Sh. milioni 30 lakini mkalipa Sh, milioni tatu ina maana nikipiga hesabu ongezeko la fedha ni Sh milioni 40. Hizo ndizo zinakupa uhalali wa kuomba Sh. milioni 460?" alihoji Makonda.

Awali, Temu alisema walipatiwa Sh. bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa shule ya wasichana ya mkoa wa Arusha na ilitakiwa kukamilika Machi, mwaka huu. Majengo yote yamekamilika isipokuwa bwalo la chakula ambalo zinahitajika Sh milioni 460 ili kukamilika.

Makonda alisema mradi huo wa shule una sintofahamu nyingi ikiwamo mhandisi kutaka nyongeza ya fedha zaidi ya mara mbili na kamati ilikataa kutoa fedha. Alisema nyongeza ya fedha hizo ambazo mhandisi wa ujenzi amekuwa akizitaka ni ukiukaji wa taratibu za ununuzi.

"Mkuu wa shule ametuambia hapa mara mbili kuwa mara ya kwanza walitaka nyongeza ya Sh, milioni 29 maana yake mara ya pili ikawa wanataka tena Sh. milioni 37. Ukijumlisha unapata Sh. milioni 66. Inawezekana tukawa tunaongezea hela kidogo kidogo. Ulishawahi kuona mtu mtaalamu wa kuua chura huwezi kuua chura ukimwekea maji ya moto kwa mpigo anaruka?

"Wataalamu waliona wakiongeza zaidi ya asilimia 15 watabanwa na sheria ya ununuzi inayokataa inataka utangaze tenda upya. Wakagundua hii staili ya kumwekea chura maji ya moto wataruka kwa wakati mmoja wakaona wapige Sh, milioni 27, Sh. milioni 29 na Sh. milioni 37 ukijumlisha bado kuna changamoto," alisema. .

Makonda alimwagiza Katibu Tawala wa Mkoa (RAS) kuunda timu ya uchunguzi kwenye miradi yote ya Longido ili apate majibu sahihi.

"Sitaki aje kiongozi wangu nikose majibu. Hivi ninavyowabana na mimi nina mabosi wangu wa kunibana, wacha niwapelekee moto kabla sijapigwa moto. Naomba nisaidiwe kuundwa kwa timu na ndugu zetu wa TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) ili tupate picha kamili ya nani wa kwenda naye," alisema.

Alisema anashindwa kumhukumu mtu kwa sababu namba zinatofautiana huku akimpongeza mkuu wa shule kuwekewa Sh. bilioni tatu za ujenzi wa shule.

Makonda alimuuliza mkuu wa shule mara yake ya mwisho kuwekewa fedha nyingi ni Sh. ngapi akasema ilikuwa Sh. Sh. milioni 50.

"Mwalimu kazi yake ni kufundisha lakini alipatiwa jukumu lingine. Haikuwa kazi rahisi sasa tukipita kwenye nyaraka tuone kila fedha iliyotoka shilingi kwa shilingi uwe na maelezo. Timu inayokuja mwalimu naomba usiniangushe,"alisema

## Bilioni 190.7/- kuimarisha elimu sekondari visiwani Z'bar

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imepanga kutumia Sh. bilioni 190.7 katika kuimarisha programu ya elimu ya sekondari.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhamed Mussa, aliyasema hayo jana wakati akiwasilisha bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2024/25.

Alisema, kati ya fedha hizo Sh. 107,410,933,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida zikiwamo Sh. bilioni 13.6 kwa ajili ya matumizi mengine na Sh. bilioni 83.2 kwa kazi za maendeleo.

Lela alisema hadi kufikia Aprili, mwaka huu, jumla ya Sh. bilioni 156.4 sawa na asilimia 82 zilipatikana.

Alisema mapendekezo hayo yanaimarisha uongozi na usimamizi wa elimu katika ngazi zote za elimu zikiwamo skuli, wilaya, mkoa na wizara.

Pia alisema fedha hzi zinalenga kuimarisha mfumo wa tathmini ya maendeleo ya elimu ya wanafunzi katika ngazi zote za elimu na kupandisha ufaulu wao kuimarisha miundonmbinu ya elimu

Aidha, alisema malengo mengine ni kujenga madarasa 1,500 kupitia ujenzi wa shule za ghorofa, shule za chini na kukamilisha madarasa yaliyoanzishwa na wananchi kwa Unguja na Pemba, nyumba 20 za walimu, ofisi ya wizara, ofisi nne za elimu wilaya, vyoo 300, dakhalia nane zikiwamo dakhalia za wanaume za Chwaka, Tumbe na Paje Mtule pamoja na kuzifanyia ukarabati mkubwa na mdogo skuli 100 za msingi na sekondari. Pia kujenga karakana elimu ya amali

"Skuli (shule 33 za sekondari Unguja na Pemba, karakana tatu kwa kila wilaya na kujenga uzio katika Skuli ya Sekondari ya Hasnuu Makame na Mohamed Juma Pindua kujengwa," alisema.

Alisema kipaumbele kingine ni kuimarisha matumizi ya tekonolojia katika kufundishia na kujifunzia kwa kuziunganisha na mkonga wa taifa taaasi za elimu zikiwemo; skuli 217 za sekondari, vituo vya walimu 12 na vituo vya ubunifu wa kisayansi (hubs) 22 pamoja na kuzipatia vifaa vya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Waziri huyo alisema katika kuendelea kutekeleza mtaala mpya wa umahiri kwakuwapatia walimu mafunzo na vifaa vya kujifunzia na kufundishia vikiwemo vya Watoto wenye mahitaji maalumu.

"Kuimarisha Mafunzo ya Ufundi na Amali kwa vyuo vitano vya Mafunzo ya Amali, utanuzi wa Chuo cha Karume (KIST) na ujenzi wa chuo cha ubaharia na kuzipatia vifaa," alisema.

Pia alisema fursa ya upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar kuanzia ngazi ya diploma pamoja na kuanza mradi wa kujenga kampasi ya kudumu ya Chuo cha IIT Madrasa; Ujenzi wa Jengo la Skuli ya kilimo, Jengo la maabara ya Sayansi ya kisasa - SUZA, Ujenzi wa skuli ya Afya, skuli ya meno na kliniki yake -SUZA.

Kipaumbele kingine, alisema ni kuimarisha huduma za maktaba kwa kuanza kujenga na kuimarisha maktaba mpya ya kisasa pamoja na maktaba mtandao (e-library).

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Waamuzi ongezeni umakini, Fair Play lala salama Ligi Kuu

**RAUNDI** ya 29 ya Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kuchezwa leo katika viwanja 15 tofauti hapa nchini huku pazia la ligi hiyo kwa msimu wa 2023/2024 likipangwa kufungwa rasmi ifikapo Mei 28, mwaka huu.

Hata hivyo tayari, Yanga inayofundishwa na Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, imeshatangazwa kuwa mabingwa wapya wa msimu huu, wakibeba taji hilo kwa mwaka wa tatu mfululizo.

Mabingwa hao watafunga pazia kwa kuvaana na Tanzania Prisons wakati Simba itawaalika JKT Tanzania huku Coastal Union itawaalika KMC na Dodoma Jiji FC itawafuata Mashujaa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika ulioko mkoani, Kigoma.

Mechi nyingine zitakuwa ni kati ya Ihefu dhidi ya Mtibwa Sugar wakati Namungo watakuwa nyumbani kuwakaribisha Tabora United, Singida Fountain Gate ikikabiliana na Kagera Sugar na Azam FC watawafuata Geita Gold kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyankumbu iliyoko mkoani, Geita.

Baada ya bingwa kujulikana kabla ya mechi hazijamalizika, zimebakia vita vya kuwania nafasi ya pili ambayo inagombewa kati ya Azam na Simba, kila moja akiwa na pointi 63 kibindoni, lakini 'Wauza Lambalamba' wakiwa juu kutokana na kuwa na idadi nzuri ya mabao ya kufunga.

Vita nyingine iliyobakia ni ya timu zinazopambana kujiepusha na janga la kushuka daraja huku Mtibwa Sugar yenye pointi 21 na inayoburuza mkia, ikionekana kabisa imekalia kuti kavu kwa sababu ikinusurika kushuka daraja moja kwa moja, basi itaangukia kucheza mechi za mtoano.

Ukiondoa Mtibwa Sugar, timu nyingine kuanzia kwa Kagera Sugar, JKT Tanzania, Singida Fountain Gate, Dodoma Jiji, Mashujaa FC, Tabora United na Geita Gold, lolote linaweza kutokea kwao endapo zitashindwa kupata matokeo chanya kwenye michezo yake miwili iliyobakia ili kumaliza msimu.

Ili kila timu inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara ivune ilichopanda, huu ni wakati wa waamuzi na wasimamizi wote wa michezo ya hatua ya lala salama kuhakikisha wanatekeleza vyema majukumu yao.

Waamuzi watakaopewa dhamana ya kuchezesha mechi hizo mbili (raundi ya 29 na raundi 30), kila mmoja akatafsiri vyema sheria na kuongeza umakini ili kutoipendelea timu yoyote kwa sababu kufanya hivyo kutawanyima haki wale wanaostahili kuondoka na pointi.

Katika mechi za hatua ya lala salama, timu kupata pointi moja iwe nyumbani au ugenini ni jambo muhimu sana katika kusaidia harakati za kujinasua na janga la kushuka daraja lakini pia zitawafanya wale walioko katika mapambano ya kufikia malengo kufaulu.

Kuchezesha kwa upendeleo wa aina yoyote kutazinyima haki timu ambazo zimewekeza katika maandalizi ya mchezo, hivyo huu ni wakati wa waamuzi sio tu kuchezesha kwa kusimamia kanuni zinazowaongoza, lakini wanatakiwa kukumbuka filimbi zao zinaweza kuharibu au kuziangamiza timu.


Waamuzi wanatakiwa kuchezesha katika viwango bora hatimaye kila timu kumaliza msimu kwa kuvuna kile ilichopanda na isitupe lawama kwa maofisa hao hali ya kuwa haikuwa na kikosi imara cha kushindana.

Lakini ili waamuzi wafanye vyema kazi zao, wachezaji wanatakiwa kuonyesha nidhamu wakati wote wa mchezo na kwa kufanya hivyo kutawasaidia kupambana kupata pointi muhimu katika dakika hizo 180 zilizobakia za kumaliza msimu huu.

Katika kuhakikisha haki inatendekea au Fair Play kama ilivyozoeleka katika soka, huu ni wakati wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kuongeza wasimamizi wa mchezo kwa sababu ya kuhakikisha hakuna 'makandokando' ya aina yoyote yanafanyika kwenye hatua hii ya lala salama.

Tunaamini kwa usimamizi bora, timu zinazostahili kushuka daraja zitapatikana kihalali lakini pia kila upande utapokea kile ilichokipanda kwa msimu mzima.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

## Ushauri, mtazamo wa Gamondi ufanyiwe kazi kukuza soka Bongo

**AKIZUNGUMZIA** alichokiona kwenye soka la Tanzania mwaka mmoja baada ya kuishi nchini, Kocha Mkuu wa Yanga raia wa Argentina, Miguel Gamondi alibainisha vitu mbalimbali ambavyo vimelifanya soka la hapa nchini kupiga hatua, lakini pia akabainisha mapungufu kadhaa ambayo alitaka yafanyiwe kazi.

Kwanza kabisa alipongeza na kusema soka la Tanzania limekuwa na si kama ilivyokuwa huko nyuma, lakini akabainisha sababu kubwa kuwa ni ujio wa wachezaji wa kigeni wenye uwezo mkubwa, ambao wamekuwa wakimiminika nchini kutokana na uwekezaji unaoendelea kufanywa kwenye klabu za hapa nchini.

"Wachezaji wa kigeni ni muhimu mno kuwepo nchini kwa sababu hawa wanaocheza ligi wameongeza chachu kubwa ya ushindani kwa wazawa, na hata vijana kuchota ujuzi, wamelichangamsha na kuliheshimisha soka la Tanzania," alisema kocha huyo kwa tathimini yake ya msimu mmoja ambao amekaa nchini akiwa kocha wa Yanga.

Kwa kauli hii ni kwamba viongozi wa soka la Tanzania, hasa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), wanatakiwa kuliona hilo kwa jicho la tatu.

Ni kwamba bila wachezaji wa kigeni, hata timu zetu za Simba na Yanga zisingekuwa zinafika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, pia wachezaji wa Kibongo wangeendelea kubweteka kama ilivyo kawaida yao, lakini kwa sasa timu ya taifa ya Tanzania, Taifa Stars, imeanza kuwa tishio kwenye michuano mbalimbali na sababu hasa, pamoja na kuwa na wengi wanaocheza soka la kulipwa, lakini wazawa wamekuwa na viwango vya juu kwa sababu ya kupigania namba na wageni katika klabu zao nchini.

Nashauri kuwa msimu ujao sasa, wageni waongezwe kutoka 12 hadi 15, yaani iwe nusu kwa nusu.

Changamoto alizoziona ni Simba, Yanga na Azam tu kutawala ligi na hii akasema si afya katika ukuaji wa soka.

"Natatizwa na ushindani kwenye ligi, kwa sababu ni timu tatu tu ndizo zenye ushindani na zenye uwezo mkubwa kuliko zingine, kuna utofauti mkubwa kati ya timu tatu za juu na zinazofuata chini ya msimamo, labda ni suala la bajeti, lakini natamani misimu ijayo kuwe na mabadiliko ushindani kutoka nafasi kwenye klabu zingine, kuwe na uwiano wa ushindani na si hivi," alisema kocha huyo.

> **Gamondi pia alizungumzia mafunzo kwa makocha wa Kitanzania, pamoja na kuibua vipaji vya vijana, kitu ambacho ameona ni changamoto kubwa nchini.**

Hili ni suala ya uwekezaji zaidi, lakini klabu za Ligi Kuu zinazoitwa au kujiita ndogo, nazo zinatakiwa kusaka wadhamini ili kupata wachezaji bora na wenye viwango vya hali ya juu.

Utashangaa kuona timu ya Ligi Kuu, lakini wachezaji wake kwenye miaka ya 1980 hadi 1990, wangekuwa wanacheza Ligi Daraja la tatu.

Gamondi amezungumzia tatizo la viwanja ambavyo alisema vinawakwaza walimu wa soka nchini

"Viwanja bado vina changamoto, navyo vifanyiwe kazi, kukiwa na viwanja vizuri kunatoa nafasi kwa wachezaji kuweza kucheza vizuri na makocha kuweza kufanya kazi kwa uhakika zaidi, ikiwemo kupata mafanikio," akasema.

Hili tayari Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), ameshalitolea ufafanuzi kuwa msimu ujao watavifungia viwanja ambavyo havikidhi vigezo, na vile ambavyo miaka nenda rundi vimekuwa hivyo hivyo, haviendelei kuboreshwa.

Gamondi pia alizungumzia mafunzo kwa makocha wa Kitanzania, pamoja na kuibua vipaji vya vijana, kitu ambacho ameona ni changamoto kubwa nchini.

Nadhani serikali, TFF na wadau, wana sehemu ya kuanzia kuyafanyia kazi yote aliyoyasema kocha huyo ambaye amesafiri nchi nyingi kwa kazi yake ya ukocha na ameonyesha maeneo ambayo wanamichezo, hususan soka, wanaweza kuyafanyia kazi kwa ajili ya maendeleo ya mchezo huo.

# Mawaziri, taasisi kutoa msimamo uvuvi Afrika

**Na Restuta James**

MAWAZIRI, taasisi za kikanda, asasi za kiraia na kampuni zinazojihusisha na uvuvi mdogo barani Afrika, wanatarajiwa kukutana kwa siku tatu nchini katika mkutano utakaotoa msimamo wa bara la Afrika kuhusu sekta hiyo.

Mkutano huo utafanyika mwezi ujao na Rais Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega, alisema lengo la mkutano huo ni kubadilishana uzoefu, kujadili mbinu za kisasa za kuwasaidia wavuvi wadogo, namna ya kukabili uvuvi haramu na hatima ya uvuvi mdogo barani Afrika.

Alisema nchini wavuvi wadogo wanachangia asilimia 95 ya uvuvi wote unaofanyika kila mwaka kuanzia baharini hadi kwenye maziwa na mabwawa.

Alisema takwimu zinaonyesha kwamba takribani Watanzania milioni sita wanategemea uvuvi mdogo, ambao unachangia asilimia 1.9 ya pato la taifa na kuiingizia nchi zaidi ya Sh. bilioni 509 ya fedha za kigeni kila mwaka.

Ulega alisema takwimu za mwaka jana zinaonyesha kwamba zaidi ya mazao ya majini ya Sh. trilioni 3.4 yalivuliwa wakiwamo samaki wa maji baridi tani 479,976.6.

"Tutabadilishana maarifa, kipi kimepitwa na wakati na tufanyeje ili hii rasilimali iwe endelevu. Mkutano utaangazia maadhimisho ya miaka 10 ya mwongozo wa uvuvi mdogo na muundo wa kisera wa kusimamia uvuvi na ukuzaji viumbe maji barani Afrika," alisema.

Waziri Ulega alisema mkutano huo utaangazia pia fursa zilizopo kwenye uchumi wa bluu kwenye sekta ya uvuvi na ufugaji wa viumbe wengine wa majini pamoja na mnyororo wake wa thamani.

"Utakuwa chachu ya kubadilishana uzoefu, fikra, njia za kisasa za uvuvi, namna ya kuufanya uwe endelevu na kupambana na uvuvi haramu. Tutakuwa na mjadala kuhusu kuwasaidia vijana na wanawake kwenye programu ya jenga kesho iliyo bora (BBT), kupitia uvuvi," alisema Ulega.

"Mkutano huu utafungua fursa za uwekezaji kwenye sekta ya uvuvi, wigo wa masoko ya nje ya mazao yetu ya uvuvi na kuongeza uwanda mpana wa wavuvi wetu kujifunza namna ya kuendesha shughuli zao kisasa ili uvivu wao uwe na tija," alisema.

Alisema ujio wa mkutano huo umetokana na jitihada za Rais Samia kuifungua nchi kidiplomasia na kwamba ni mara ya kwanza kufanyika nchini.

Kwa mujibu wa Waziri Ulega, mkutano huo utahudhiriwa na wavuvi wadogo wa baharini, maziwa na mabwawa pamoja na taasisi za kifedha.

# Mikakati yaandaliwa kulinda mifugo asili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeanza mikakati ya kuhakikisha mifugo ya asili wakiwamo ng'ombe aina ya Ufipa haipotei nchini kwa kuanzisha vituo viwili vya kuhifadhi mifugo hiyo.

Moja ya mikakati hiyo ni pamoja na kuanzisha vituo vya Kongwa na West Kilimanjaro kwa ajili ya kuhifadhi mifugo ya asili na kwamba Kongwa inahifadhi mbari za ng'ombe wa asili na West Kilimanjaro inahifadhi mbari za mbuzi na kondoo wa asili.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti, alisema hayo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Kalambo (CCM), Josephat Kandege, aliyetaka kujua serikali ina mpango gani wa kuhakikisha mbegu za ng'ombe wa asili ya Ufipa hazipotei.

Akijibu swali hilo, Mnyeti alisema katika kuhakikisha mifugo ya asili, wakiwamo ng'ombe aina ya Ufipa haipotei, wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) ilianzisha vituo vya Kongwa na West Kilimanjaro kwa ajili ya kuhifadhi mifugo hiyo.

Alisema kituo cha Kongwa kinahifadhi mbari za ng'ombe wa asili na kituo cha West Kilimanjaro kinahifadhi mbari za mbuzi na kondoo wa asili.

"Mkakati mwingine unaotekelezwa na Wizara wa kuhifadhi mifugo ya asili ni kuvuna na kuhifadhi mbegu za mifugo ya asili ikiwemo mbari aina ya ufipa katika kituo cha Taifa cha Uhimilishaji cha NAIC – Arusha," alisema Mnyeti

Kadhalika, alisema katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara imepanga kununua madume nane (8) ya ng'ombe wa asili aina ya ufipa, Gogo, Iringa red, Singida white, Ankole, Tarime, Sukuma na Maasai kwa ajili ya kuvuna mbegu na kuanza uhifadhi wa vinasaba vya mbari za mifugo ya asili iliyo hatarini kutoweka hapa nchini.

**Akijibu swali hilo, Mnyeti alisema katika kuhakikisha mifugo ya asili, wakiwamo ng'ombe aina ya Ufipa haipotei, wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) ilianzisha vituo vya Kongwa na West Kilimanjaro kwa ajili ya kuhifadhi mifugo hiyo.**



Nguzo ya umeme ikiwa imewekewa viroba vya mchanga ili isianguke baada ya eneo ilipochimbiwa kuchimbika na maji kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika eneo la Kivule, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Benki zajipanga kufungua matawi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

Serikali imesema Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imetoa idhini kwa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kufungua tawi katika eneo la Konde wilaya ya Micheweni kisiwani Pemba na matayarisho ya kufungua tawi hilo yanaendelea.

Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, alisema hayo jana bungeni, jijini hapa, wakati akijibu swali la Mbunge wa Micheweni, Abdi Hika Mkasha, aliyetaka kujua serikali ina mpango gani wa kurejesha huduma za kibenki za CRDB, NMB na PBZ katika wilaya ya Micheweni.

Chande alisema Benki za CRDB, NMB na PBZ kwa sasa hazina matawi katika wilaya ya Micheweni na wananchi wa wilaya hiyo wanapata huduma za kibenki kutoka katika benki hizo kupitia mawakala 27 wa CRDB (11), NMB (12) na PBZ (wanne).

"Kabla ya benki kufanya uamuzi wa kufungua tawi jipya, benki husika hufanya upembuzi yakinifu ukiwa na lengo la kuangalia kama kuna uwepo wa biashara ya kutosha ambayo italeta faida kwa benki husika" alifafanua Mhe Chande.

Aliongeza kuwa serikali inatambua ukuaji wa uchumi katika wilaya ya Micheweni na kuwa benki za CRDB, PBZ na NMB zitaendelea kufanya utafiti na upembuzi yakinifu ili kuona uwepo wa tija katika wilaya hiyo ili kuweza kufungua huduma za kibenki.

# Sababu ongezeko uraibu dawa za kuleva zaanikwa

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

SABABU ya kuongezeka kwa waraibu wa dawa za kulevya katika mkoa wa Tanga, imetajwa kuwa ni kutokana na kuwapo mpakani, hivyo kuwa na njia za panya kupenyeza mihadarati hiyo.

Lakini pia wasafirishaji ambao wanatumika kulipwa dawa hizo kama ujira wa kusafirishia ni sababu nyingine ambayo inaongeza watumiaji katika maeneo hayo kwa kuwa hawana mahali pa kwenda kuuzia.

Kaimu Kamishna wa Kinga na Tiba wa, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Dk. Casian Nyandindi, aliyasema hayo kwenye mkutano wa wadau wa huduma za waraibu (MAT) mkoa wa Tanga uliofanyika jijini hapa.

"Tulijua mkoa wa Dar es Dalaam unaongoza kwa kuwa una watu wengi lakini Tanga inaongoza kwa matumizi ya dawa za kulevya. Tunapaswa kuwapa elimu ya kutosha juu ya madhara ya dawa hizi,

"Dawa hizi zinachangia kwa kiasi kikubwa kusababisha tatizo la afya ya akili. Lakini pia wako wenye tatizo hili ambao wanakwenda kutumia dawa za kulevya. Tusikate tamaa kuwaelimisha wale ambao bado hawajazidiwa ukimsaidia mraibu umesaidia jamii nzima," alisema.

Dk. Nyandindi alibainisha kwamba matumizi ya dawa za kulevya ni mtambuka, hivyo kila mmoja anapaswa kuwajibika kwa kufuata taratibu, kanuni na sheria katika kutimiza wajibu wake.

Naye daktari wa magonjwa ya akili ambaye pia ni Mkuu wa Kitengo cha Dawa za Methadone, Dk. Wales Karata, alisema mkoa umepata athari kubwa kutokana na ongezeko la matumizi ya dawa hizo.

"Serikali imeona waraibu walipo waweze kupatiwa dawa, na wale ambao wameitika na kuanza dawa wanaendelea vizuri na maisha wakiwa na familia zao,

"Tuna asas za kiraia ambazo zinapambana na waraibu katika mitaa yao, lakini bado tunahitaji Taasisi mbalimbali ziweze kuliona hili na kuweza kuwa msaada kwa hawa waraibu" alisema.

Meneja wa Wadau wa Huduma za Waraibu (MAT) Mkoa wa Tanga, Dk. Otmar Massawa, alisema wamejipanga kuhakikisha wanaongeza jitihada katika kushuhulikia kwa ufanisi matumizi mabaya ya dawa za kulevya.

Dk. Massawa aliwasilisha taarifa ya maendeleo ya mpango huo tangu kuanzishwa kwake iliyobainisha kuwa wapokea huduma 1,113 walijiandikisha na 683 wanaendelea na huduma.

Alibainisha kwamba kwa kiasi kikubwa wamefanikiwa kubadilisha maisha ya watumiaji wa dawa za kulevya lakini kuna tatizo la ukosefu wa vituo vya kutolea huduma hizo.

"Hata hivyo nina imani kwamba, mkutano huu utatoa furaha kwa wadau wa MAT mikoani hapa na kujadili matatizo yaliyopo ikiwa ni pamoja na kumtafuta suluhu ili kupunguza madhara katika jamii ambayo yanawakabili waraibu wa dawa za kulevya," alisema.

Kwa upande wa waraibu wanaopokea huduma, walitoa ushuhuda kuhusu maisha yao ya uraibu na jinsi MAT ilivyowasaidia kurudi katika maisha yao ya kawaida.

Mkutano huo umewezeshwa na Shirika la Tanzania Health Promotion Support (THPS) chini ya mradi wa Afya Hatua unaofadhiliwa na Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kupambana na UKIMWI (PEPFAR), kupitia Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa cha Marekani (US CDC).



Mkurugenzi wa Mradi wa Afya Thabiti unaotoa Huduma na Matibabu ya VVU wa Amref Tanzania, Dk. Edwin Kilimba akizungumza wakati wa mkutano wa utambulisho wa mradi huo kwa kitengo cha Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe cha Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), jijini Dodoma, hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Somo la Historia, Maadili kuanzishwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema somo jipya la Historia ya Tanzania na Maadili, litakalofundishwa kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita, litabeba maudhui yanayolenga kumjenga Mtanzania kuwa mzalendo na mwajibikaji.

Somo hilo pia litamfanya kijana wa kitanzania kuifahamu historia, desturi, mila na maadili ya nchi.

Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, alisema hayo jana bungeni wakati akijibu swala la Mbunge wa Viti Maalum, Najma Giga (CCM).

Giga katika swali hilo, alitaka kujua kwa nini serikali isiweke kwenye mitaala somo la uraia na uzalendo ili kizazi kijacho kiwe na uelewa wa haki na wajibu wa raia nchini.

Akijibu swali hilo, Kipanga alisema serikali kwa kutambua umuhimu wa kutoa elimu ya uraia na uzalendo kwa kizazi cha sasa na kijacho, ilifanya maboresho ya Mitaala ya Elimu Mwaka 2023 ambapo katika maboresho hayo, tayari maudhui kuhusu elimu ya uraia na uzalendo yameingizwa.

Aidha, alisema kupitia somo jipya la Historia ya Tanzania na Maadili, litakalofundishwa kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita, litabeba maudhui yanayolenga kumjenga Mtanzania kuwa mzalendo na muwajibikaji anayefahamu historia, desturi, mila na maadili ya Kitanzania.

**Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, alisema hayo jana bungeni wakati akijibu swala la Mbunge wa Viti Maalum, Najma Giga (CCM).**

# Waziri wa viwanda ataka kasi ukaguzi wa mizani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Shaaban, ameitaka Wakala wa Vipimo (WMA) kuongeza kasi ya ukaguzi kwa watu wanaochezea mizani ili kuhakikisha wananchi wanapata bidhaa kwa thamani ya fedha.

Omar aliyasema hayo juzi alipotembelea banda la WMA baada ya kufungua maonyesho ya Wiki ya Viwanda na Biashara yanayofanyika katika viwanja vya Bunge yakiwa na lengo la kutoa elimu kwa wabunge kuhusu majukumu na kazi zinazofanywa na taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Alisema ni muhimu kwa taasisi hiyo kufanya ukaguzi mara kwa mara ili kuwabaini na kuwachukulia hatua kali wafanyabiashara ambao wamekuwa wakiwapunja wanunuzi kwa kuchezea mizani.

Kadhalika, alipongeza WMA kwa kuendeleza ushirikiano na taasisi ya Wakala wa Vipimo Zanzibar (ZAWEMA) na kuahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa taasisi hizo mara kwa mara ili kuhakikisha zinatimiza lengo kuu ambalo ni kumlinda mlaji kupitia matumizi sahihi ya vipimo.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Alban Kihulla, alisema kupitia maonyesho hayo yaliyoandaliwa na Wizara ya Viwanda na Biashara, wabunge mbalimbali wametembelea banda la wakala na kupata ufahamu kwa undani majukumu ya taasisi hiyo hususani katika maeneo ya uhakiki wa dira za maji na alama.

Akitoa elimu kwa wabunge, Kihulla alisema kwa mujibu wa sheria ya WMA Sura Na. 340 mazao yoye ya shamba yanatakiwa kufungashwa kwa uzito usiozidi kilogramu 100 na endapo gunia litafungashwa kwa uzito zaidi ya ule unaokubalika kisheria, hatua zitachukuliwa dhidi ya msafirishaji na mmiliki wa mzigo.

Kihulla alisema WMA inaendelea kuwasihi wafanyabiashara na wamiliki wote wa vipimo kuhakikisha vipimo vyao vinakuwa sawa kila mara ili kutenda haki wakati wote bila kuwapunja watumiaji wa huduma katika maeneo yao.





# Wabunge vijana wanolewa usalama kazini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAMLAKA ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA) imetoa mafunzo ya usalama na afya kazini kwa wabunge 100 chini ya Umoja wa Wabunge Vijana Tanzania (TYPF).

Mafunzo hayo ni utekelezaji wa mkakati wa taasisi hiyo kuhakikisha makundi mbalimbali katika jamii yanakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu kanuni bora za usalama na afya mahali pa kazi.

Mafunzo hayo yalitolewa juzi jijini hapa na kufunguliwa na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, akimwakilisha Waziri wake, Deogratius Ndejembi.

Akifungua mafunzo hayo, Katambi alisema OSHA ina wajibu mkubwa wa kulinda nguvu kazi ya taifa hususan vijana ambao ndio wanaunda asilimia kubwa ya nguvu kazi inayotumika katika uzalishaji nchini na duniani kote.

"Kazi kubwa ya serikali kupitia OSHA ni kuwalinda wafanyakazi ili wasipate ajali, magonjwa au vifo vitokanavyo na kazi kwani kunapokuwa na wagonjwa wengi maana yake serikali inapata mzigo mkubwa wa kuwahudumia, hivyo kuathiri uchumi wa nchi kutokana na fedha nyingi kutumika kununua madawa na vifaa tiba pamoja na uzalishaji kushuka kutokana na nguvukazi kupungua na muda wa uzalishaji kupotea kwa kuuguza wagonjwa," alisema Katambi.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Vijana Tanzania (TYPF) ambaye pia ni Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia Elimu, Zainab Katimba, alisema lengo la semina hiyo lilikuwa kuwajengea uelewa wabunge vijana katika eneo la usalama na afya mahali pa kazi.

"Kupitia mafunzo haya tumejifunza mengi hususan dhana ya vihatarishi katika maeneo yetu ya kazi na tahadhari zinazopaswa kuchukuliwa. Hivyo, tutakuwa katika nafasi nzuri zaidi kuendelea kuishauri serikali pamojanakuwashirikishaelimuhii wananchi wetu," alisema Katimba.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema mafunzo hayo ni mwendelezo wa mkakati wa Taasisi ya OSHA kuyafikia makundi mbali mbali nchini na kuyajengea uelewa wa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi.

Alisisitiza kuwa mafunzo ya usalama na afya ni muhimu kwa wafanyakazi wote nchini hususan vijana ambao ndio washiriki wakubwa katika shughuli za uzalishaji ambapo tafiti mbali mbali ukiwemo utafiti uliofanywa na OSHA mwaka 2022 zinaonesha kwamba vijana ndio wanaoathirika zaidi na ajali na magonjwa mahali pa kazi.

## Bashungwa aagiza mabadiliko sheria

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, ameishauri Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) kuirejesha bungeni sheria inayowasimamia kama wanaona ina upungufu ili ifanyiwe marekebisho yatakayoiwezesha kuwa na meno kwa wale wote wanaokiuka taratibu.

Bashungwa alitoa agizo hilo juzi jijini hapa, alipokuwa akifungua mkutano wa mwaka wa mafundi sanifu.

Alisema endapo bodi hiyo inaona sheria waliyo nayo ina upungufu, ni vyema kuipeleka bungeni ili kufanyiwa marekebisho.

Alisema lengo la kusema hivyo ni kutaka kuwaweka sawa wahandisi ili waweze kufanya kazi zao kwa ufasaha na ufanisi pale wanapopata zabuni mbalimbali.

"Angalieni sheria yenu vizuri kama mnaona ina upungufu basi iwasilisheni bungeni ifanyiwe marekebisho yatakayosaidia kuwa na makali ya kuwawajibisha wanaokiuka taratibu," alisema Bashungwa.

Aidha, alisema wahandisi wote wanatakiwa kujisajili ili waweze kutambulika ikiwemo kujiunga na wenzao kwa ajili ya kufanya kazi mbalimbali za miradi.

Kadhalika, alisisitiza suala la wahandisi kujisajili katika Bodi yao na kuongeza kuwa waliosajiliwa watumie kiapo vizuri katika ufanyaji kazi zao.

Katika hatua nyingine Bashungwa alisema wahandisi 2,785 waliosajiliwa idadi hiyo ni ndogo, hivyo wanapaswa kuhimiza watu wajisajili ili watambulike.

Waziri Bashungwa pia aliisisitiza bodi hiyo kuwawajibisha wahandisi wanaokwenda kinyume na taratibu na sheria za kazi na kuongeza kuwa wasipofanya hivyo watakuwa wanalea wahandisi waharibifu.

Msajili wa ERB, Bernard Kavishe, alisema bodi hiyo itaendelea kuwawajibisha wahandisi wanaokwe da kinyume na taratibu za kazi kama ilivyo ada.

Alisema mkutano huo wa sita wanakwenda kujadili mambo muhimu ambayo yanakwenda kuimarisha utendaji wa kazi zao za kila siku. Pia aliwataka wahandisi kila mmoja kusikiliza kwa makini,ikiwemo kutoa maoni yao pale wanapohitajika kufanya hivyo.

"Naomba msikilize kwa makini kile mnachofundishwa kwenye mkutano wenu na mtoe maoni," alisema Mhandisi Kavishe.



Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Maganga (wa pili kulia), akizungumza na wajasiriamali na wananchi wa wilaya ya Iramba, mkoani humo juzi, waliokuwa wakipatiwa elimu ya fedha na watumishi wa Wizara ya Fedha, ikiwa ni kutekeleza mpango wa Serikali wa kutoa elimu ya fedha kwa wananchi wote nchini. Wengine ni Ofisa Usimamizi wa Fedha, kutoka Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Elizabeth Mnzava (kushoto), Ofisa Usimamizi wa Fedha wa Idara hiyo, Salim Kimaro (wa pili kushoto) na Ofisa Maendeleo ya Jamii Ofisi ya Rais TAMISEMI, Avelina Kapologwe. **PICHA: WF**

# Watumishi waonywa kushiriki siasa

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

WATUMISHI katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida wamehadharishwa kujihusisha na masuala ya kisiasa na badala yake wajikite katika kufanya kazi kulingana na taaluma zao kwa ajili ya maendeleo ya wilaya na taifa kwa ujumla.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, James Mkwega, alisema hayo jana wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Alisema watumishi wana jukumu la kusaidia kuleta maendeleo kwenye halmashauri kwa kutumia taaluma zao na kwamba kuanza kujihusisha na masuala ya kisiasa ni jambo ambalo linaweza kuwasababisha wasiweze kutekeleza vyema majukumu yao.

Aidha, Mkwega aliwataka madiwani kushiriki pamoja katika kukusanya mapato kwa maendeleo ya halmashauri na kwa taifa kwa ujumla.

"Uhai wa halmashauri ni mapato, tunapata shida sana tunaposikia kata fulani inalalamikiwa kutorosha ushuru,sheria hizi tunazopitisha ni za kulinda mapato hivyo tuwaelimishe wananchi wetu tutii hizi sheria kwa sababu tunajenga nchi yetu," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Asia Messos, aliwakumbusha madiwani kuweka kipaumbele katika kukomesha suala la utoro kwa wanafunzi shuleni.

"Changamoto ya utoro katika wilaya yetu imekuwa ukubwa, kwa leo nawaomba madiwani walibebe suala hili katika ajenda zao ili kuhakikisha wanafunzi watoro wanapatikana," alisema.

**Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, James Mkwega, alisema hayo jana wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2023/24.**





# Wataka mabadiliko katika sheria ya habari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WADAU wa habari na waandishi wa habari visiwani Zanzibar, wameitaka serikali ya Zanzibar kuharakisha mchakato wa mabadiliko ya sheria ya habari ili iendane na wakati uliopo na pia kuleta mageuzi katika sekta hiyo.

Hayo waliyasema katika maadhimisho ya uhuru wa vyombo vya habari ambayo Zanzibar iliadhimisha jana na kuwakutanisha waandishi wa habari, wadau wa habari pamoja na watetezi wa haki za binadamu.

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanazania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa Ali, alisema bila kupatikana kwa sheria madhubuti zitakazowalinda wanahabari, ni vigumu kufanya kazi zitakazoleta mabadiliko katika jamii.

Alisema miongoni mwa changamoto za waandishi wa habari ni kukosa ulinzi na heshima kutokana na sheria zinazotumika kuwa za muda mrefu na zimepitwa na wakati.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Ernest Sungura, alisema tasnia ya habari Tanzania inahitaji ushirikiano baina ya wadau wa habari na serikali ili kufanikisha mabadiliko ya sheria ambazo zinakwaza utendaji wa kazi za kihabari.

Pia alisema changamoto kubwa kwa waandishi wa habari ni masuala ya kiuchumi kutokana na ukuaji wa teknelojia wa vyombo vya kidigitali ambavyo vinakua kwa kasi kubwa.

Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC), Abdallah Abrahman Mfaume, alisema maadhimisho hayo ni mwendelezo wa mikutano ya kitaaluma inayolenga kutoa fursa kwa wadau kujitathmini na kuweka mikakati ya kuimarisha taaluma hiyo.

Alisema tasnia ya habari ina changamoto nyingi zinazohitaji uwapo wa sheria zinazoendana na mabadiliko ya teknolojia na kwamba ndiyo sababu ya waandaaji wa kongamano hilo waliteua kaulimbiu isemayo 'Uhuru wa Vyombo vya Habari na Mageuzi ya Sera na Sheria za Habari Zanzibar'.

Naye Katibu Mtendaji wa Tume ya Utangazaji Zanzibar, Suleiman Abdallah Salim, alisema serikali imepokea mapendekezo ya mabadiko ya sheria za habari kutoka kwa wadau wa habari ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi.

Pia alisema ni vyema kutambua kuwa mabadiko ya sera na sheria yanahitaji mchakato ambao kwa sasa umefika kwa mwanasheria mkuu na inategemea kuwasilishwa katika baraza la wawakilishi ili kusomwa kwa mara ya kwanza.

Alisema taaluma ya habari ni eneo nyeti linalopaswa kuangaliwa na kuongozwa na sheria, hivyo ni vyema waandishi wa habari wakafuata maadili yaliyowekwa bila kuvuka mipaka ya sheria.

# Kamera ulinzi kuwekwa maeneo ya hoteli

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohamed, amesema serikali ya Zanzibar inakusudia kutekeleza mradi mkubwa wa kuweka miundombinu ya kamera za ulinzi katika maeneo yote ya ukanda wa hoteli za kitalii ili kudhibiti matukio ya uhalifu.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi visiwani hapa wakati akijibu hoja za wajumbe wa baraza hilo waliochangia makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2024/25.

Alisema kwa sasa serikali iko katika hatua za kufanya upembuzi yakinifu katika kutekeleza mradi huo muhimu ambao utalinda mali za wawekezaji katika hoteli za kitalii.

Kwa mujibu wa Waziri, jukumu la kuweka ulinzi ni pamoja na kuwahakikishia wawekezaji usalama wa miradi yao ni la serikali ndiyo maana uamuzi uliofikiwa ni kuja na mradi wa kuweka kamera za kudhibiti matukio ya uhalifu.

Aliyataja maeneo ambayo yatahusika na uwekaji wa miundombinu ya kamera za ulinzi ni Nungwi ambako kunaongoza kwa kuwapo kwa miradi mingi ya hoteli za kitalii.

Maeneo mengine ni Kiwengwa, Pwani Mchangani na mkoa wa Kusini Unguja ambako kasi ya ujenzi wa miradi ya hoteli za kitalii inaendelea.

"Mheshimiwa Spika, napenda niwajulishe wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuweka kamera za ulinzi katika ukanda wote wa miradi ya hoteli za kitalii kwa ajili ya kudhibiti matukio ya uhalifu," alisema.

Hata hivyo alisema serikali imeanza kuchukua hatua za kukabiliana na matukio ya uhalifu ikiwamo kuanzisha kikosi cha polisi wa utalii ambacho kinafanya kazi katika maeneo yote ya ukanda wa hoteli za kitalii.

Alisema kwa kiasi kikubwa kikosi hicho kimefanikiwa kudhibiti matukio madogo yaliyokuwa yakijitokeza yakiwamo ya uporaji wa mali za watalii na vifaa vyao kama kamera.

"Mheshimiwa Spika kwa kiasi kikubwa tumefanikiwa kudhibiti matukio ya uhalifu ikiwamo watalii kunyang'anywa vitu vyao kwa kuja na kikosi cha polisi utalii ambacho kimesaidia kwa kiasi kikubwa," alisema.



Daladala maarufu chai maharage, ikiwa imepakia mzigo mkubwa juu huku kondakta wake akining'inia katika eneo la Michenzani, mjini Zanzibar jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SMZ kuwekeza zaidi wataalamu wa afya

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imeeleza azma ya kuwekeza katika wataalamu na madaktari bingwa kwenye hospitali mpya za wilaya na mikoa ili kuwapunguzia gharama wananchi wanaofuata matibabu nje ya nchi hasa kwa maradhi ya moyo, saratani, uti wa mgongo na ubongo.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar alipozungumza na Dk. Suzan Homeida, raia wa Sudan anayefanyia kazi nchini Rwanda.

Dk. Mwinyi alimueleza Dk. Homeida kwamba Zanzibar inahitaji ushirikiano wa kina kwa madaktari bingwa na wataalamu katika maeneo manne ya afya ikiwamo wataalamu na madaktari bingwa wa upasuaji wa moyo, saratani, mfumo wa mishipa ya fahamu inayohusisha uti wa mgongo na ubongo.

Alisema serikali hutumia fedha nyingi na watu wanatumia gharama kubwa kufuata huduma hizo nje ya Zanzibar hasa India, Uturuki na Kenya.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi alimweleza Dk. Homeida kuangalia uwezekano wa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hasa kwenye kuongeza nguvu kwa hospitali ya Mkoa ya Lumumba ambayo inahitaji wataalamu wenye weledi wa ubobezi wa hali ya juu kwenye maeneo hayo,

Dk. Mwinyi aliongeza kuwa licha ya serikali kufanya uwekezaji mkubwa wa miundombinu na vifaa vya kisasa kwenye hospitali hiyo, bado inahitaji wataalamu wabobezi.

Pia alimtaka mtaalamu huyo kuangalia uwezekano wa kuwapata wataalamu na madaktari bingwa kutoka Sudan kwa vile ana uzoefu nao wa muda mrefu hata wataalamu wa kawaida ili kuongeza nguvu kwenye hospitali za wilaya za Unguja na Pemba kwa kuendelea kulisukuma gurudumu la afya kwenye uwekezaji mkubwa wa sekta hiyo.

Naye Dk. Homeida alipongeza serikali ya Zanzibar kwa mafanikio makubwa yaliyofikiwa hasa kwenye sekta ya afya na kusifu hatua ya ujenzi wa hospitali za kisasa za wilaya na Mikoa zenye miundombinu na vifaa vya kisasa baada ya kuzitembelea akiongoza na timu ya uongozi wa Wizara ya Afya chini ya Waziri mwenye dhamana, Nassor Ahmed Mazrui.

Dk. Homeida aluiiahidi serikali kushirikiana nayo ili kuendeeza sekta ya afya, Zanzibar.

Akizungumzia utalii, amesifu uzuri wa visiwa na fursa zilizomo zinazotokana na sekta hiyo akieleza matumaini yake makubwa kwa vivutio vya utalii akilenga zaidi utalii wa afya kwa miaka ya baadaye.

Aidha, alisema ana mengi ya kufanya kwa bara la Afrika ikiwemo Zanzibar akiwa na ndoto ya kuanzisha chuo kikubwa zaidi cha afya Dar es Saalam baada ya Chuo Kikuu cha Sayansi ya Tiba na Teknolojia cha Khartoum, Sudan.

Vilevile, Dk. Homeida alisema kuwapo kwake Zanzibar kutampatia uzoefu mpya wa kutengeneza mafanikio zaidi ya kukuza sekta ya afya visiwani hapa hasa kwenye hospitali mpya za wilaya.

Dk. Homeida ni daktari mshauri mkuu wa magonjwa ya damu na Mkurugenzi Mkuu wa taasisi ya "Frontierpoly21" iliyoko Kigali, Rwanda na aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Chuo Kikuu cha Sayansi ya Tiba na Teknolojia Khartoum.



**NAMELESS AWALINDA WATOTO WAKE** Ukurasa 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI MEI 25, 2024



# Watu ninawakosa

HATIMAYE mwimbaji maarufu wa Pop duniani, Celine Dion, amezungumzia maisha yake na kueleza ana wakati mgumu wa kukubaliana na ugonjwa unaomsumbua.

Tangu 2022, Celine anapambana na ugonjwa usio wa kawaida unaoshambulia neva za mwili unaojulikana kama stiff-person. Kupitia filamu yake mpya inayoitwa I Am Celine Dion, mwanamuziki huyo aliweka bayana picha ambazo hazijawahi kuonekana katika kipindi chake cha kwanza.

Pia amezungumza kwa undani ugonjwa wake huo na namna anavyopambana nao.

Amesema awali hakuwa tayari kusema chochote kuhusu afya yake, lakini kwa sasa ameona kuna umuhimu wa kuweka wazi.

"Ninafanya kazi kwa bidii kila siku lakini lazima nikubali, imekuwa mpambano mgumu. Ninakosa sana. Watu. Ninawakosa," alisema. Ikiongozwa na Irene Taylor, msanii huyo anayependwa kutokana na vibao vyake vitamu vya kimahaba, amesema bado anaamini sauti yake inaendesha maisha yake.

"Sauti yangu ni kondakta wa maisha yangu, ingawa hivi majuzi imekuwa ngumu." alisema

Hata hivyo, ameonyesha matumaini kwamba ipo siku atasimama na ataweza kuimba tena.

"Ninawakumbuka sana watu nawakosa, nisipoweza kukimbia nitatembea, nisipoweza nitatambaa na sitaacha sitaacha kujaribu," aliendelea kusema huku akitokwa na machozi.

Dion alikiri kwamba anapata furaha kwa kufanya ubunifu wake mwenyewe na kuwatumbuiza mashabiki wake.

BASI SAWA

## Davy Machords hapindishi maneno



MTAYARISHAJI maarufu wa muziki wa Bongo Fleva, Davy Machords, amesema suala la wizi wa muziki limekuwa la kawaida na hakuna mwanamuziki ambaye anaweza kusema yeye ni msafi.

Akizungumza hivi karibuni, Davy Machords, amesema amekuwa akitumika sana na Cosota kushughulikia kesi mbalimbali za aina hiyo na kwamba ongezeko la wizi halifanyi muziki wa Bongo Fleva kushuka.

"Hata kwa muziki wa nje kuna baadhi wameiba mapigo ya nyimbo za kwetu na sisi tumechukua kwao, lakini tatizo hili huwezi kusema kwamba muziki wetu umeshuka, bali umezidi kuimarika," amesema



## Nameless awalinda watoto wake

MKONGWE wa muziki nchini Kenya, Nameless, amesema kila siku anawalinda watoto wake kuhusu maudhui yasiyofaa katika mitandao ya kijamii.

"Hata kwa familia yangu, ninawalinda sana watoto wetu. Lazima niendelee kuwaambia na kuelewa mambo kama chuki na kwamba sio kila mtu anakutakia mema, hata wakati mimi sipo. Wanaelewa maisha hayo." Alisema Nameless.

Aliendelea kusema kuwa amewafanya watoto wake waelewe yeye baba yao ni mtu mashuhuri, na anakabiliana na changamoto nyingi kwani na wao wapo ambao wanaweza kuwachukia.



## Mnazaleti anataka ku'lala'

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Suma Mnazaleti, hatimaye ametambulisha wimbo wake mpya unaoitwa 'Lala' ambao umeanza kurushwa hewani jana.

Video ya wimbo huo ambao amemshirikisha Lody Music, umeonekana kuwapagawisha mashabiki wa muziki.

"Namshukuru Mungu kwa kuja na ujio mpya wa kibao changu cha lala, naamini mashabiki wangu wataupokea na kuniunga mkono katika kazi hii ambayo nimendaa kwa muda mrefu ili iwe bora zaidi," amesema Mnazaleti.



## G Nako atoa somo

RAPA maarufu nchini G Nako, amesema kufanya muziki wa jukwaani ni kazi ngumu kama msanii hatafanya mazoezi ya kutosha.

Amesema wanamuziki wengi hawapendi mazoezi na ndio maana kupiga muziki wa jukwaani kwa kutumia vyombo imekuwa ngumu kwao.

"Kupiga muziki kwa vyombo ni ngumu kama hautafanya mazoezi, hili ndilo tatizo la wasanii wengi wa hapa nchini ambao hawawezi kupanda jukwaani na kutumbuiza. Jambo la muhimu kuingia katika aina ya muziki huu kwani inamjenga mwanamuziki kuwa imara na mwenye uwezo," amesema G nako.

## Ngoma tano kali kupongeza wachezaji

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Yanga imetwaa ubingwa wa soka Tanzania Bara, baadhi ya wasanii wapo mbioni kutoa nyimbo za kuipongeza.

Kwa miaka ya karibuni baadhi ya wasanii wa kizazi kipya wamekuwa wakitoa nyimbo za kuzisifia klabu zinazotwaa ubingwa, kufanya vizuri kwenye michuano mbalimbali, au kuzihasisha tu.

Wasanii wakubwa kama kina Diamond Platnumz, Ali Kiba, Marioo, na wengineo wameshatoa ngoma kadhaa zinazohusiana na klabu za soka, hususan, Simba na Yanga.

Hii ni tofauti kidogo na miaka kadhaa nyuma ambapo wasanii wa bongo fleva hawakuwa wanatunga nyimbo zinazohusu soka, iwe timu za klabu ya timu ya taifa, lakini kwa sasa kumekuwa na mwamko huo, kama ilivyokuwa miaka ya 1970, hadi mwishoni mwa miaka ya 1980, ambapo wanamuziki wa dansi walifanya kazi kubwa kutunga nyimbo zinazopongeza timu za mpira wa miguu na wachezaji wake.

Bendi zilikuwa zinaimba kusifia hata timu za mikoa ambazo bendi hizo zipo na hasa zile zilizokuwa zikitwaa Kombe la Taifa kwenye michuano ya Taifa Cup.

**Yanga Bingwa (Western Jazz)**

Yanga ambayo msimu huu imetwaa tena ubingwa, ilitungiwa wimbo wa bendi maarufu ya Western Jazz baada ya kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara kwa miaka mitano mfululizo kuanzia mwaka 1968, hadi 1972.

Katika wimbo huo, wachezaji wanaoimbwa humo ni kina Abdurahman Juma, Adam Chipukizi, Baraka Kitenge (Baba yake mzazi mtangazaji Maulid Kitenge na wengineo.

**Hongera Simba (Baba Gaston)**

Baba Gaston Ilunga wa Ilunga, mkongomani aliyekuwa akipiga muziki nchini Kenya, alitunga kibao cha kuisifia Simba baada ya kutwaa Kombe la Afrika Mashariki na Kati kwa mara ya kwanza mwaka 1974 ambalo kwa sasa linaitwa Kombe la Kagame.

Katika kibao hicho aliwataja wachezaji kadhaa ambao walicheza mechuano hiyo kama Athumani Mambosasa, Shaaba Baraza, Mohamed Kajole, Omari Chogo, Adam Sabu, Abdallaah Kibadeni na wengino.

**Taifa Stars (Orchestra Safari Sound)**

Mwanzoni mwa miaka ya 1980, bendi ya Orchestra Safari Sound chini ya Fred Ndala Kasheba ilitoa kibao walichokiita 'Taifa Stars'. Ilikuwa ni baada ya wachezaji wa timu hiyo kutishia kujiuzulu baada ya kufungwa bao 1-0 na timu ya taifa ya Uganda.

Kibao hicho kiliwaasa wasijiuzulu na waendelee kulipambania taifa na kweli, timu ikaenda ugenini na kushinda mabao 3-1, mawili ya Zamoyoni Mogella na moja la Celestine 'Sikinde' Mbunga.

**Wanasoka (Mbaraka Mwinshehe)**

Mbaraka Mwinshehe na bendi ya Morogoro Jazz Band alitoa kibao kiitwacho 'Wanasoka' ambacho kilikuwa ni kuwapongeza wachezaji wa timu ya mkoa wa Morogoro ambacho kilitwaa Kombe la Taifa mwaka 1970.

Baadhi ya wachezaji waliotajwa humo ni Kapteni Jongo, Mnyepe, Sembuli, Manga, Rajab, Chogo, Shomari, Njenje, Sabu na wengineo.

**Taifa Cup Tanga-Atomic Jazz Band**

Bendi ya Atomic Jazz haikuwa nyuma. Nayo ilitoa kibao ikilipa kile cha Morogoro Jazz, baada ya timu ya mkoa wa Tanga kutwaa Kombe la Taifa mwaka 1973.

Wachezaji waliotajwa humo ni kwa jina moja moja ni Hemed, Makunda, Salim, Mwabuda, Zimbwe, Mbwana, Sharrif na wengineo waliolitwaa kombe hilo.





## Mwiko: Baba, mtoto humo humo

**Na Adam Fungamwango**

SIKU ZOTE mapenzi ni ugonjwa. Anayependa haoni hasikii. Kwenye pengo huita kuna mwanya na kwenye chongo huona kuna kengeza. Lakini pamoja na hayo yote, kupenda pia kuwa mipaka yake. Huwezi kumpenda mke wa mtu. Huwezi kumpenda ndugu yako wa damu, au mtu mwenye nasaba nawe. Na yeyote anayefanya hivyo, mwisho wake huwa ni majuto.

Filamu ya 'Mwiko' inathibitisha hili. Imechezwa na wasanii Mohamed Nurdin maarufu kama 'Chekibudi', Madebe Lidai, Anwar Nassao, Shasta na wengineo.

Inaanza kwa kuonyesha Maisara na Medebe ni mtu na mpenzi wake. Hata hivyo hilo linapingwa mno na familia ya kina Maisara ambao hawataki uhusiano huo.

Mwisho wa siku anapigwa na kaka ya Maisara na kualazwa hospitalini.

Baada ya kutoka, kunakuwa na uhasama kati ya ukoo wa Madebe na Maisara. Ugomvi huo unasababisha hata lile wazo la Madebe kutaka kupeleka barua kwa mpenzi wake kufa.

Hiyo inampa fursa mzee mmoja kijijini hapo anayeitwa Jitikavu kupeleka ombi la kutaka kumuoa binti huyo. Pamoja na kwamba ana umri mkubwa, watoto na mabinti  wakubwa kuliko binti huyo, lakini wazazi wa Maisara wanakubali haraka kwanza wakitaka binti yao aolewe, lakini pia ni kama kumkomoa Madebe.

Ndoa inafungwa, Madebe bado akili yake iko kwa Maisara. Kitendo hicho cha mara kwa mara kukutana na mpenzi wake wa zamani, kinamfanya mume mzee Jitikavu kutokuwa na amani. Mara kwa mara anakwenda nyumbani kwa Madebe kwenda kumuwekea mkwara.

Hatimaye Maisara anapata ujauzito. Anampa siri shoga yake kuwa ujauzito huo si wa mumewe mzee Jitikavu na wala si wa mpenzi wake Madebe. Wa nani?

Shoga mwenyewe naye mbea hatari. Maneno hayo anayapeleka kwa wahusika. Kiguu na njia hadi kwa Madebe na pia akamweleza yote mumewe mzee Jitikavu.

Akawa tayari ameshakaanga mbuyu akawaachia wenye meno watafune. Mume na Madebe kila mmoja kivyake akawa anatafuta ukweli hiyo ni ya nani?

Maisara apanga kukutana na mpenzi wake aliyempa mimba ili wayapange. Shoga yake alikuwa ameshaijua sehemu hiyo, hivyo akawapa taarifa Jitikavu na Madebe.

Kila mmoja alifika na kumshuhudia Maisara akiwa na Anwar, mtoto wa mzee Jitikavu wa kumzaa mwenyewe. Kumbe ndiye mwenye mimba.

Kumbe pia binti huyo alikuwa na uhusiano wa kimapenzi wa Anwar tangu zamani, hivyo baba yake alipomuoa alikuwa kama amemsogezea hivi.

# Ben huwezi kuficha ukweli




MWIGIZAJI maarufu wa Hollywood, Ben Affeck, amejikuta akiwa katika wakati mgumu kwa wapiga picha, baada ya kuonekana akificha mkono wake kwa kitambaa kuhofia kuonekana vidole vyake vya mikono.

Tukio hilo limetokea juzi wakati akitoka nje ya jengo la shule huko Los Angeles wakati alipokwenda kumchukua mwanawe Samweli.

Hivi karibuni kumeibuka uvumi kwamba Ben na mkewe mwanamuziki Jenifer Lopez, wametengana na kila mmoja ameamua kuacha kuvaa pete ya ndoa mikononi mwao.

Picha zilizosambaa mitandaoni zinaonyesha Ben akificha mkono wake wa kushoto kwenye sweta yake.



## Cassie asema neno

ALIYEKUWA mpenzi wa rapa maarufu wa Marekani, P Diddy, Cassie ameamua kuzungumza baada ya video kuvuja ikionyesha akipokea kipigo kutoka kwa msanii huyo.

Hata hivyo, Cassie ameonekana kuwa mwangalifu katika maneno kutokana na makubaliano aliyofikiana na Diddy mahakamani kumaliza jambo hilo.


"Asante kwa upendo na usaidizi wote kutoka kwa familia yangu, marafiki, wageni, na wale ambao bado sijakutana nao. Kumiminika kwa upendo kumeunda nafasi kwangu kutulia na nijisikie salama sasa, lakini huu ni mwanzo tu, unyanyasaji wa majumbani ni suala ambalo lilinivunja moyo," amesema Cassie.

## Pole Flavour, yote ya Mungu

MKALI wa muziki wa Afrobeats, Chinedu Okoli, maarufu kama Flavour, amethibitisha kuwa baba yake mzazi amefariki dunia.

Flavour kupitia ukurasa wake wa Instagram, alichapisha video akionyesha wakati baba yake alipokuwa hai akiwa amekaa kwenye kiti cha magurudumu huku yeye akiwa amekaa karibu yake akipiga gitaa na kumuimbia nyimbo.

Hata hivyo hakueleza chanzo cha kifo cha mzee huyo, lakini katika ujumbe wake msanii huyo alimuelezea alikuwa nguzo na muhimili wake katika shughuli zake za muziki.





## Tiwa una uhakika?

MWANAMUZIKI kutoka Nigeria, Tiwa Savage amesema watu wa taifa hilo wana mioyo ya ujasiri na ni bora kwa kila kitu.

Akizungumza na kituo cha redio cha Uingereza, Kiss Fresh, amesema anajivunia kuwa Mnigeria kwa sababu ni watu maalum na wanaoacha alama popote duniani.

"Hata kama wewe ni dereva wa teksi au mwalimu wa shule, daktari au kazi yoyote. Sisi ni bora kwa chochote tunachofanya na ninahisi kama tuna ujasiri ndani yetu kufanya katika uwanja wowote tulio nao," amesema.

## Banky upo makini

MWANAMUZIKI na mwanasiasa wa Nigeria, Banky W, ameshauri kwamba maisha halisi ni yale ya kutofuata maoni ya watu katika mitandao ya kijamii.

Wakati akiwa katika mahojiano, Banky W amesema yeye na mkewe Adesua Etomi-Wellington wamefanikiwa kuwa na maisha ya faragha kutokana na kujifunza kutotawaliwa na mawazo ya watu wengine.

Amesisitiza kwamba watu hawatakiwi kutafuta uthibitisho wa maisha yao kutoka kwenye mitandao kwa kupitia maoni yanayotolewa wanapochapisha ujumbe au picha.





# Wadau 600 kushiriki maonyesho ya utalii

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

ZAIDI ya wanunuzi 600 wa utalii kutoka nchi 40 duniani na waonyeshaji pamoja na wadau 468 wa utalii kutoka nchi 37, wamethibitisha kushiriki maonyesho ya kimataifa ya Karibu -Kilifair yanayotarajiwa kuanza Juni 7 hadi 9, mwaka huu jijini Arusha.

Vilevile, wadau hao na wanunuzi wa utalii watatembelea vivutio vya utalii, ili wakawe mabalozi wazuri kwenye nchi zao.

Akizungumza jana jijini Arusha, Mkurugenzi wa Kilifair Ltd, ambao ni waandaaji wa maonyesho hayo, Dominic Shoo, alisema lengo la maonyesho hayo ni kutangaza vivutio vilivyopo nchini na wakauze nchini kwao.

"Siku hizi tatu tunatarajia kuwa na kiwango kikubwa cha biashra kwa sababu lengo letu kubwa kukutanisha wadau toka mataifa mbalimbali duniani, kuja kujua vivutio vyetu hapa Tanzania, wavitembelee na kuweza kuwa mabalozi wazuri, kwa ajili ya kuuza vivutio vya Tanzania," alisema.

Alisema mwaka huu onyesho hilo ni kubwa kuliko la mwaka jana, sababu wamekua na waonyeshaji zaidi na mwamko wa wanunuzi ni mkubwa kuliko mwaka jana na wamekua na kiwango cha juu, kuliko mwaka jana kutokana na vitu ambavyo wameweza kuvinunua, ili kuhakikisha onyesho hilo linalingana na hadhi ya viwango vya kimataifa.

Aidha, alisema Juni, 8 watakuwa na tamasha la muziki utakaoleta watu pamoja na utakuwa wa kiwango cha kimataifa kutokana na kushirikisha wataalamu wa burudani.

"Kwa sababu siku hizi tatu tumeona tutakuwa na wageni wengi Arusha, lakini hawana burudani ya kutosha tukaona kuliko wakapate burudani sehemu tofauti, ambazo hazina hadhi tumeamua kuwaandalia kitu kipya kitakachowapa burudani Juni nane mwaka huu,hapa hapa viwanja vya Magereza na tumeunga na wataalamu wa burudani tunashirikiana nao," alisema.

Hata hjvgo alisema utalii unakua na kwamba ambapo msimu huu wa utalii umefunguka mapema ukilinganisha na mwaka jana, ina maana huhitaji wa kiu ya kwenda kwenye hifadhi ni mkubwa.

"Lakini watu wana hoteli mpya nyingi na wanabishara mpya, wanataka juhakikisha wengi wanazijua na kupitia hapo wajue taarifa zao na bei zake,"alisema

Kwa mujibu wa Shoo, maisha sasa hivi ni Afrika, ukienda nje ya nchi onyesho lolote linalokosa Mtanzania wanashtuka, sababu Afrika nkombozi wao Tanzania kwenye sekta ya utalii.

Aliyataja baadhi ya mataifa hayo yafakayoshiriki knyesho hilo, kati ya 40 wanakotoka wanunuzi wa utalii kuwa ni Ujerumani, Amerika, Italia, nchi za Afrika Mashariki, Aftika Kusini na Asia.

Maonyesho hayo yanatarajia kufunguliwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki.

Mkuu wa kitengo cha masoko na mauzo, kutoka kampuni ya Media Works, Noel Petro, aliiomba serikali kuruhusu ujenzi wa mabanda ya maonyesho ya kudumu, ili kuwepo kwa mazingira salama nyakati zote, badala ya kusubiri wakati wa onyesho tu.

"Kutokana na maonyesho haya ni ya kipekee kwetu sisi, yanaleta fursa ya utalii kwani wateja wetu wakubwa zaidi ya asilimia 70 wanatokana na utalii."alisema.



Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT) wilaya ya Babati mjini, mkoani Manyara, Eva Makilagi Luoga (wa tatu kulia), akikabidhi kadi ya uanachama wa UWT kwa mkazi wa mtaa wa Maisaka, Magdalena Ombay alipofanya ziara katika eneo hilo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# RC Makonda ashangaa mradi wa maji wa mil. 600 kutofanya kazi

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, amepigwa butwaa na kushindwa kutoa uamuzi baada ya kukuta mradi wa kisima cha maji kilichojengwa kwa Sh. milioni 600 hakitoi maji katika kijiji cha Ilidonyo, kata ya Sinya wilayani Longido.

Kutokana na hali hiyo, amemwagiza Meneja wa Wakala ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mhandisi Ramadhani Musiba, kuandika barua kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji kwa kitendo cha kumdangaya mbele ya wananchi na hayuko tayari kufanya naye kazi.

Makonda akiwa kwenye ziara katika wilaya ya Longido jana, alibaini changamoto mbalimbali jambo ambalo lilimshangaza hasa wananchi kutokunufaika na mradi wa maji wa Sh milioni 600.

Makonda alihoji kuhusu Sh. bilioni 520 ya mradi wa maji uliohusisha uchimbaji wa visima 56 ambao kimoja ndicho cha Longido, kwa nini hakijawekewa usanifu wa usambazaji maji kwa wakazi wa eneo hilo.

"Nataka kujua ni umbali gani umetumika kusambaza maji jiji la Arusha na kushindwa kusambaza maeneo ya Namanga ambapo umbali wa Kilomita 35 na eneo hili la Longido ndipo kisima kimojawapo kilipo umbali wa kilomita 1.9 ili kusambaza maji kwa wananchi iweje maji yasifike kwa wananchi,"alisema

Msimamizi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha (AUWSA) Wilaya ya Longido, Mhandisi Upendo Shusho, alikiri kisima hicho kutowanufaisha wananchi kwa kuwa bado kuna vifaa vinahitajika.

Makonda alionyesha wazi kusikitishwa kwa kuwa katika mradi huo mkubwa wa Sh. bilioni 520 kulikuwa na mtandao wa usambazaji maji wa kilomita 900 ndani yake lakini cha kushangaza hakuna kilichofanyika tangu kisima kikamilike mwaka jana.

Aidha, Makonda alimtaka Meneja Musiba kumwandikia barua Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji kuhusiana na kutoa taarifa ya uongo na kusisitiza kuwa hayuKo tayari kuendelea kufanya naye kazi.

Makonda alifikia uamuzi huo baada ya Mwenyekiti wa Kijiji cha Lemereta, Supuk Melita, kueleza kumekuwa na changamoto ya maji kwa wananchi na zahanati wanayoitegea katika kijiji cha Lemereta.

Alisema tayari wameshatoa taarifa kwa zaidi ya miezi mitatu na alikwenda ofisini kwao kuwajulisha hakuna hatua zilizochukuliwa na kuendelea kuteseka.

"Mheshimiwa Makonda walivyokusikia unakuja kutembelea ndio jana wamepita huku na pikipiki utazani wamekuja kufanya patro lakini ni zaidi ya miezi mitatu nimewapa taarifa kuhusiana na hiki kisima hawajaja kutusaidia ili tupate maji," alisema Melita.

"Tunakuomba utusaidie tupate maji tunaelekea kipindi za kiangazi hapa mabomba yamepasuka na maji yanamwagika hakuna ufuatiliaji hili tatizo ni la muda na kuunga bomba halihitaji bajeti ni ufundi tu wabishe ni lini wamekuja katika huu mwaka,"alisema

Makonda alimhoji Musiba mara yake ya mwisho kufika kijijini hapo ni lini alimjibu kuwa ni wiki mbili zilizopita.

"Kwa hiyo haya maji kumwagika hadi inafika hatua twiga hawezi kupita je ni uongo?" alihoji Makonda

Ofisa huyo alikiri taarifa zilizotolewa ni za ukweli na Makonda kumwambia inaonyesha dhairi kuwa ukaguzi wa miradi haufanyiki.

Melita alisema alimjulisha kwa kumuandikia barua na kumpigia simu na hawezi kudanganya ni jambo ambalo lipo wazi.

Makonda aliendelea kumkomalia meneja huyo na kusema: "Mzee unanitaka nichukie kuna mwingine amesema hili jambo ni la muda mrefu wa miezi sita na mwenyekiti kaja mpaka ofisini kwako wewe unatuambia ulikuja wiki mbili yaani kwa umri wako unaona fahari kutudanganya,"

"Mzee unatosha kweli kuwahudumia wananchi kama umekuwa muongo kiasi hicho unanidanganya mbele yangu alafu unakataa hii nafasi yako umeipataje."

Musiba alimueleza kuwa nafasi yake ameipata kwa uteuzi kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Maji.

"Sasa mtafute Katibu Mkuu umwambie Makonda kasema sifai kuwa msimamizi wa mradi wa maji Longido. Nataka mtu anayethamini kazi anayopewa, mtu anayelinda uhai wa maji nataka gharama zinazoeleweka na usimamizi mzuri wa mradi mwambie leo Katibu Mkuu kuwa Makonda kasema hanitaki na sifai na umweleze sababu kubwa ya kunikataa mimi ni mwongo nimemdanganya mbele ya wananchi na wananchi wamethibitisha kuwa mimi ni mwongo," alisisitiza.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Hawa ndiyo waliosababisha vijana wa zamani kujiita'mabitozi', sasa 'matozi'




**Na Adam Fungamwango**

SIKU hizi kijana akiwa anapenda kuvaa vizuri na mtanashati anaitwa au kujiita 'tozi.'

Vijana wa kisasa wanapenda kuitwa au kujiita 'matozi', ikiwa na maana kwanza ni kijana anayejipenda, mtanashati, anajua kuvaa na mara zote ni nadhifu na msafi, ambapo kwa jina lingine wanaitwa 'mabishoo.' Hata hivyo wenyewe huwa hawapendi kuitwa jina la 'bishoo', badala yake wanalipenda sana lile la 'tozi.'

Nini maana ya jina hilo na limetoka wapi? Nani aliyewapa jina hilo vijana watanashati?

Jina hilo ni mwendelezo wa jina la 'mabitozi', lenye maana ile ile ya mwanzo.

Vijana wa zamani, kuanzia miaka ya katikati ya 1960, hadi mwishoni mwa miaka ya 1990, wao walijiita au kuitwa, 'mabitozi.'

Sababu ya kuitwa au kujiita hivyo ni ile ile, kujipenda, kuvaa vizuri, utanashati, umaridadi, usafi na unadhifu.

Zamani miaka hiyo, ukionekana uko nadhifu, umevaa vizuri, watakuita 'bitozi.'

Hapa unapata picha kuwa kumbe maneno 'mabitozi' na 'matozi' yana maana moja, tofauti ni enzi tu, na staili ya mavazi tu. Vijana wa zamani wao walijiita 'mabitozi' na wa sasa, 'matozi.'

Hawa wa kisasa 'wamelieditti', tu neno 'bitozi', wakaweka 'tozi.'

Sasa twende pamoja, hilo jina la 'bitozi', mpaka kuwa 'tozi' limetokana na nini, hapo vijana watanashati, wenye kujipenda wanalitumia?

Vizazi vyote hivi, vya zamani na sasa wanatumia neno hilo ambalo ni jina la bendi ya muziki ya vijana machachari wa zamani, waliounda kundi lao nchini Uingereza katika jiji la Liverpool, wakaliita, 'The Beatles.' Sasa nadhani umeanza kupata picha jina hilo limetoholewa kutoka wapi.

Waswahili wao wakaacha kulitaja kama 'bitozi', wakaita kama wanavyoita, na baadaye likabadilika na kuwa 'tozi' hadi hii leo.

The Beatles lilikuwa kundi la wanamuziki wanne, ambao ni John Lennon, Paul McCartney, George Harrison na Richard Starkey, maarufu kama Ringo Starr.

wakati huo walikuwa vijana wadogo, Waingereza waliojaliwa vipaji vya kuimba miaka hiyo, wakiwa na umri mdogo tu kuanzia miaka 18 mpaka 22, lakini walikuwa balaa.

Jamaa pamoja na kujaaliwa kuimba, walikuwa wasafi, wanajua kuvaa, kujipenda na kutokana na utanashati wao, ndiyo Wabongo walipoanza kujiita au kuitwa 'mabitozi' kwa wale vijana walionekana wanatashati, na hadi leo hii hawanaitwa 'matozi.'

Nadhani sasa vijana wa kizazi kipya ambao walikuwa hawaelewi neno 'tozi' limetoka wapi, sasa wameelewa.

Wao ndiyo waliolipaisha sana jiji la Liverpool na Uingereza kwa ujumla, muziki wao ulipata soko duniani na wao wenyewe kupendwa sana na kuwa ndiyo kioo cha vijana wengi duniani kutokana na utanashati wao.

Wanamuziki hawa walitikisa dunia, walipata pesa nyingi sana katika umri mdogo, walifanya chochote walichokitaka. Katika kila nyimbo 100 bora katika chati ya Billboard miaka hiyo, nyimbo kuanzia nyimbo tano au zaidi zilikuwa zao.

Chenye mwanzo hakikosi mwisho, kundi lilivunjika mwaka 1970, baada ya baadhi ya wanamuziki kujiengua na kuanza kupiga muziki kivyao, maarufu kama 'solo artist.'

Mpaka leo hii, ni wanamuziki wawili tu ambao wapo hao, nao ni McCartney mwenye umri wa miaka 81 sasa na Ringo Starr, ambaye ana miaka 83.

Lennon aliuawa New York nchini Marekani akiwa na miaka 40, Desemba 8 mwaka 1980, na Harrison, alifariki 2001, akiwa na umri wa miaka 58.

Hadi leo limeacha athari kadhaa duniani, ikiwemo hata hapa Tanzania, vijana watanashati zamani kujiita 'mabitozi' na kizazi cha sasa wanajiita 'matozi.'

**Tuma meseji 0716 350534**





Picha zote ni za kundi machachari la muziki, 'The Beatles,' lililoanzishwa mwaka 1960 na kuvunjika mwaka 1970, ambalo lilitikisa dunia.

HABARI KIMATAIFA

# Marekani kuipa Kenya hadhi mshirika mkuu

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani, Joe Biden ametangaza kuwa anashirikiana na Bunge kuiteua Kenya kuwa mshirika mkuu asiyekuwa mwanachama wa Nato kwa ajili ya kuimarisha ushirikiano wa kiusalama.

Kiongozi huyo alisema nchi hizo mbili zina wasiwasi sawa wa usalama katika kupambana na kundi la Islamic State (ISIS), msaada kwa Ukraine dhidi ya uvamizi wa Russia na kuweka utulivu nchini Haiti.

Rais Biden alizungumza hayo wakati akizungumza na Rais wa Kenya, William Ruto, katika Ikulu ya nchi hiyo ya White House.

Ruto alisema ushirikiano huo utainua mchango wa nchi yake katika uimarishaji wa amani katika pembe ya Afrika.

Pia alisisitiza kuwa serikali yake itajitolea kuongoza ujumbe wa Kimataifa wa kusaidia kurudisha usalama nchini Haiti.

Kenya itakuwa taifa la kwanza la Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kuteuliwa kuwa mshirika mkuu asiyekuwa mwanachama wa Nato. Nchi nyingine za Afrika zenye hadhi hiyo ni Morocco, Misri na Tunisia.

Hadhi ya mshirika mkuu asiyekuwa mwanachama wa Nato huwapa washirika wa kigeni fursa ya upendeleo ya kijeshi na kiuchumi na Marekani. **BBC**



Majaji wa Mahakama ya Haki ya Umoja wa Mataifa (ICJ) wakiingia katika chumba cha mahakama kutoa hukumu katika ombi la Afrika Kusini ikiitaka kuiamuru Israel kusitisha mashambulizi katika mji wa Rafah jana. **PICHA: AFP**

# Wapalestina 60 wauawa Gaza

**GAZA,** PALESTINA

VIKOSI vya jeshi vya Israel viliendelea kufanya mashambulizi katika Ukanda wa Gaza usiku kucha wa kuamkia jana na kuwaua watu 60 katika maeneo mbalimbali.

Vyombo vya habari vilisema kuwa mashambulizi makubwa ya angani na ardhini yamefanyika katika maeneo ya mji wa kusini wa Rafah.

Ilielezwa kuwa vifaru vya Israel vilisonga mbele kusini mashariki mwa Rafah, kuelekea wilaya ya magharibi ya mji wa Yibna na kuendeleza operesheni yake katika vitongoji vitatu vya mashariki.

Shirika la habari la Reuters, lilizungumza na mkazi mmoja ambaye alisema, majeshi ya Israel yalijaribu kusonga mbele zaidi kuelekea magharibi, na sasa yapo kwenye ukingo wa Yibna, ambako kuna watu wengi.

Alisema bado hawajalivamia eneo hilo.

"Tunasikia milipuko na tunaona moshi mweusi ukitoka katika maeneo ambayo jeshi limevamia. Ulikuwa usiku mwingine mgumu sana," aliambia Reuters kupitia programu ya mazungumzo.

Israel ilianzisha mashambulizi yake Gaza kufuatia shambulio lililoongozwa na Hamas dhidi ya raia wa nchi hiyo mnamo Oktoba 7, mwaka jana na kuua watu 1,200, na wengine 250 kuchukuliwa mateka.

Wakati huo huo, shirika la wakimbizi la Norway, lilisema msaada wa kibinadamu umekuwa mgumu kupatikana kutokana na vikwazo vilivyowekwa na pande zinazopigana.

Shirika hilo limesema malori 2,000 ya misaada yamekwama upande wa Misri wa mpaka na mji wa Rafah, ambao umefungwa tangu jeshi la Israel lianzishe operesheni dhidi ya Hamas katika mji huo.

Suze van Meegen, mkuu wa operesheni wa NRC huko Gaza, alisema Wapalestina wananyimwa shehena zinazohitajika kama chakula, dawa, mahema, matangi ya maji, bidhaa za usafi na mambo mengine ya msingi.

Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF) lilisema limefungua vituo vipya, barabara za lami na kuweka mabomba ya maji ili kupunguza mateso ya Wapalestina.

Linadai kuwa watu milioni moja waliokimbia makazi yao wamehama kutoka Rafah, kabla ya mapigano.

Wakati huo huo, miili ya mateka wengine watatu wa Israel imepatikana katika Ukanda wa Gaza.

Taarifa ya jeshi hilo ilisema miili hiyo ilitambuliwa kuwa ni Hanan Yablonka, Michel Nisenbaum na Orion Hernandez.

IDF ilisema miili hiyo ilipatikana katika mji wa kaskazini wa Jabalia katika operesheni ya pamoja na shirika la kijasusi la Israel iliyofanyika usiku kucha.

Hii inakuja wiki moja baada ya miili mingine mitatu ya mateka kupatikana.

Kuna mateka 130 ambao bado wanashikiliwa na Hamas ndani ya Gaza. **BBC**

## China yaitishia Taiwan mazoezi ya makombora

**BEIJING,** CHINA

JESHI la China limewapeleka jana wanajeshi wenye vifaa vya makombora katika mazoezi ya kijeshi kuzunguka kisiwa cha Taiwan.

Kwa mujibu wa televishini ya China CCTV, kwenye jaribio hilo washambuliaji kwa kushirikiana na vikosi vya wana maji walionekana wakifanya mashambulizi yasiyo halisi ya kurusha makombora.

Kadhalika washambuliaji hao walionekana wakipanga safu yao kijeshi kwa uelekeo wa safu kadhaa za mashambulizi katika upande wa bahari wa mashariki.

Luteka hiyo ya kijeshi inafanyika ikiwa ni siku chache baada ya rais mpya wa Taiwan Lai Ching-te, kuanza kazi rasmi. Taiwan imelaani vitendo hivyo vya China.

China imekuwa ikikichukulia kisiwa cha Taiwan chenye kujitawala kidemokrasia kama sehemu yake na kumshutumu Rais Lai kama mtu anayetaka utengano. Hata hivyo, katika hotuba yake ya kwanza aliitaka serikali ya China kusitisha vitisho na kwamba pande zote mbili za bahari hazina udhibiti wa upande wowote.

Katika taarifa yake kamandi ya kijeshi ya jeshi la China kwa upande wa mashariki, ilisema mazoezi hayo yaliyopewa jina la Upanga wa Pamoja - 2024A, yana shabaha ya kujaribu uwezo wa kunyakua madaraka kwa pamoja, kuanzisha mashambulizi na kuchukua maeneo muhimu.

Ofisa mmoja mwandamizi katika masuala ya usalama wa Taiwan, aliiambia Reuters kwamba washambuliaji wa China walifanya mashambulizi ya dhihaka dhidi ya meli za kigeni katika maeneo ya karibu eneo la Bashi Channel, sehemu ambayo inaitenganisha Taiwan kutokea Ufilipino.

Ofisa huyo, ambae alizungumza bila kutaja jina lake, kutokana na unyeti wa hali ilivyo, alisema boti kadhaa za walinzi wa pwani ya China walishiriki kile kilichoitwa mashambulio ya kuitishia Taiwan kwenye pwani ya mashariki.

Lakini kwa upande wa walinzi wa pwani wa China walisema kuwa wameendesha utekelezaji wa mazoezi ya sheria katika eneo la bahari la mashariki mwa Taiwan kwa jana pekee. Wakilenga mafunzo juu ya uthibitishaji , utambuzi na tahadhari.

HABARI KITAIFA

# Tembo Warriors yasaka nafasi kombe la Dunia

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufungwa na Ghana katika hatua ya robo fainali ya Afrika (AAFCON), Kocha Mkuu wa Tembo Warriors, Salvatory Edward ameweka wazi kubadilisha malengo ya mashindano hayo na sasa anatafuta nafasi kwa ajili ya kucheza kombe la Dunia 2026.

Tembo Warriors walifungwa 4-1 na Ghana katika mchezo wa hatua ya robo fainali uliopigwa uwanja wa PetroSport, nchini Misri.

Tanzania leo inashuka dimbani tena dhidi ya mabingwa Angola kuendelea kuisaka nafasi adhimu ya kushiriki Kombe la dunia 2026 kuiwakilisha Tanzania na Afrika katika nafasi saba, zinazoenda kuiwakilisha kombe la Dunia.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Salvatory alisema mechi ya Ghana ilikuwa ya ushindani mkubwa, wachezaji walipambana lakini haikuwa bahati kwao.

Alisema licha ya kufungwa kwenye hatua ya robo fainali lakini bado wapo katika mashindano na wanajiandaa kwa mechi zijazo kutafuta nafasi ya kwenda kucheza kombe la Dunia.

"Malengo yetu yamebadilika baada ya kuhitaji kombe la Afrika, sasa tunahitaji kujipanga vizuri katika mechi zetu, mashindano magumu na tunapambana na matumaini yetu kuwa sehemu ya timu saba ambazo tutaenda kuiwakilisha nchi katika kombe la Dunia, 2026," alisema Salvatory.

Nahodha wa Tembo Warriors, Shadrack Hebron alisema wamepoteza mechi ya robo fainali na wana sahau matokeo hayo na kuweka nguvu zao kwenye mechi zijazo kutafuta nafasi ya kombe la Dunia.

"Bado hatujakata tamaa, tumepoteza mechi ya robo fainali lakini bado hatujaondolewa kwenye mashindano, sasa tunapambana kutafuta nafasi ya kufuzu na kwenda kucheza kombe la Dunia mwakani," alisema Shadrack.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo Dk. Suleiman Serera amewataka wachezaji na benchi la ufundi (Tembo Worriors) kuyachukulia matokeo waliyopata katika mechi yao dhidi ya timu ya Taifa ya Ghana.

"Tukiendelea kulia na kusikitika wala haitaturudishia kitu, tunachotakiwa kujua mwana michezo yeyote anayekuja kwenye mashindano anakuja kwa ajili ya kushinda, hakuna anayekuja kwa ajili ya kupoteza,"alisema

Aliwataka kutokuwa na simanzi bali waende kuboresha nafasi wanazozipata na kutumia katika mechi zingine, mechi za Afrika kipimo sahihi na kupambana kutafuta nafasi ya kufuzu kombe la Dunia.

Brigedia Generali Ismail Shajack Ismail mwakilishi wa Balozi wa Tanzania nchini Misri amewataka wachezaji na benchi la ufundi kwenda kujipanga vilivyo kupambania timu saba zitakazoshiriki Kombe la Dunia.



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Jumuiya ya Umoja wa Ulaya yaliyofanyika katika Makazi ya Balozi wa Umoja huo, jijini Dar es Salaam juzi jioni. **PICHA: WF**

## Shughuli za awali SGR kuanza Juni

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema shughuli za awali za treni ya umeme kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, zinatarajiwa kuanza Juni 14, mwaka huu, ili kuruhusu kuanza safari ya kwanza ya abiria kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma Julai 25, mwaka huu.

Prof. Mbarawa aliyasema hayo jana baada ya kuhitimisha ziara fupi ya kukagua ujenzi unaoendelea wa madaraja ya juu na treni ya kichwa mchongoko (EMU) katika eneo la Vingunguti, Uwanja wa Ndege na Majumba Sita mkoani Dar es Salaam.

Alisema lengo la kuanza kwa shuguli hizo ni kujiimarisha kwa mifumo yote ili kubaini dosari ambazo zinaweza kujitokeza kabla ya kuanza safari rasmi ya abiria kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma.

Pia alisema majaribio ya treni ya umeme bado yanaendelea ikiwa ni pamoja na treni ya kichwa mchongoko kilichowasili hivi karibuni.

Prof. Mbarawa alisema treni ya kichwa mchongoko itatumika kubeba abiria kutoka Dar es Salaam na kuwashusha katika vituo vikubwa vya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Tabora, Isaka na Mwanza huku kingine kikiwa cha kushusha kituo baada ya kituo.

Kuhusu ujenzi wa madaraja hayo, Prof. Mbarawa alisema kwa mujibu wa wahandisi, wamemhakikishia madaraja hayo matatu ya juu yatakamilika kabla ya Julai 10, mwaka huu, kabla ya shughuli kuanza. Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, alisema majaribio ya treni yaliyofanyika ni kwa kuzingatia sheria chini ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu Tanzania (LATRA).

Alisema sababu tatu zinazofanya shughuli za awali zianze ni kujenga uwezo na uratibu wa mifumo iwapo kuna mapungufu; kujenga imani kwa jamii kuhusu mradi na kuingiza kipato kwa shirika.

Aprili 22, mwaka huu, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alizindua majaribio ya kwanza ya treni inayotumia umeme kutoka Dar es Salaam hadi Makutopora -Dodoma iliyoshuhudiwa na zaidi ya viongozi 100 wa dini waliosafirishwa hadi Dadoma.

# Uchaguzi marudio CHADEMA Njombe waingia dosari

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

UCHAGUZI wa marudio wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo CHADEMA Mkoa wa Njombe umeingia dosari baada ya wanachama kushikana mashati na kupigana ngumi kwa madai kuwa kanuni zimekiukwa.

Hatua hiyo imesababisha Msimamizi wa Uchaguzi huo, Naibu Katibu Mkuu CHADEMA Bara, Benson Kigaila, kuondoka eneo la tukio huku akisisitiza hautaahirishwa.

Wakati uchaguzi huo ukifanyika eneo la ukumbi wa Milimani Motel mjini Njombe, ghafla wanachama kutoka wilaya za mkoa wa Njombe waliomba mwongozo kuhusu uhalali wa wajumbe wa wilaya ya Makete ambao uchaguzi wao ulikatiwa rufani makao makuu ya chama kisha kuundwa kikosi kazi.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA) Mkoa wa Njombe, Leah Masasi, alisema wanachotaka katiba isikany'agwe na kumwomba naibu katibu mkuu na kamati kuu iwaambie kwamba kikosi kazi hicho kiliundwa kwa ajili ya kukamilisha uchaguzi wa wilaya ya Makete au kupiga kura.

Naye Katibu Mwenezi wa CHADEMA Wilaya ya Wanging'ombe, Steven Gohagi, alisema wameona baadhi ya vifungu vya sheria vinakiukwa na kuanza kutoa mawazo ambayo yalikataliwa.

"Uchaguzi ulifanyika Makete kwa sababu haukuwa wa kikanuni na kikatiba. Tukamwomba msimamizi wa uchaguzi atufafanulie ili tuelewe kwa sababu chama hiki ni chama kikubwa ambacho watu wanakitegemea kije kiwasaidie. Sasa kama kiongozi mkubwa anakaidi mawazo na maoni ya viongozi wake haiko sawasawa," alisema.

Hata hivyo, alisema viongozi wanavunja katiba kwa makusudi kwa kudhani wanawaogopa.

Kuhusu viongozi wa wilaya ya Makete, walitaka kurejea kwenye katiba kama wanaruhusiwa kufanya uchaguzi.

"Kwa kujibu wa katiba yetu kama wataruhusiwa kufanya uchaguzi, wafanye. Kama katiba itakuwa inawagomea waondoke kwa sababu ni viongozi ambao hawakuchaguliwa kwa mujibu wa katiba. Wilaya ya Makete ina kata 23 ambazo zimefanya uchaguzi ni tatu tu, hivyo akidi haikutimia kwa sababu walitakiwa wafikie asilimia 50 ya kata," alisema Gohadi .

Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Wanging'ombe, Patrick Njulumi, alisema wanagomea kufanyika kwa uchaguzi huo kwa sababu ya uwapo wa wajumbe ambao si halali kupiga kura.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa kwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosababisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-**14**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

"Sasa wewe unaenda wapi na utajificha mpaka lini shemeji?" Teddy akauliza swali zuri na muhimu, lakini lilikuwa gumu.

"Mpaka sasa sina pa kwenda. Ninachofanya ni kuwakwepa tu askari, nikisubiri siku ambayo ukweli utafahamika." "Lini sasa?" Akauliza kwa nguvu na msisitizo.

Kamal, akamwambia. "Teddy, wala siyo muda mrefu, kila kitu kitajulikana. Nikwambie tu humo humo ndani ya Jeshi la Polisi, wapo askari wengi wema sana, wamesema watanisaidia ili ukweli ufahamike." Akamdanganya. Kidogo Teddy akaonekana kutulia. "Haiwezekani Damu ya Mariamu, iende hivi hivi, nakuapia, wote waliohusika watabainika. Hapo ndipo nitakuwa nimemzika Mariamu wangu, naye atakuwa amepumzika kwa amani, baada ya hapo baadaye nitatafuta mke mwingine wa kuoa. Na mke huyo ni lazima awe na vigezo kama alivyokuwa navyo Mariamu." "He! nani tena huyo?" "Ni wewe. Sitotaka kwenda kwingine, nitakuoa Teddy wewe ili kumuuenzi Mariamu." "Teddy hakuamini kama maneno hayo yanatoka kwa Kamal. Alionekana kufurahi kana kwamba itafungwa mwezi ujao.

"Nitakuombea kwa Mungu jambo hili lifanikiwe ili utimize ulichoniahidi." Akasema akianza kulia tena. Safari hii machozi ya furaha.

Waliagana na kwa tabu sana. Lakini ilibidi lazima iwe hivyo. Teddy arudi nyumbani aendelee na maisha yake, Kamal aondoke, kwenda kujificha kwa ili asikamatwe kwa kosa la kumuua mkewe.


Mpaka wakati huo, ni watu wawili tu duniani ndiyo waliokuwa wanajua kuwa Mariamu hakuuawa na mchumba wake. Ni Kamal mwenyewe na Teddy. Lakini ni nani atawasikiliza?

Tena inawezekana na Teddy akaingizwa kwenye kosa hilo kwa kuambiwa inawezekana naye alikula njama ili awe na Kamal.

Familia yao nzima ilijua kuwa ukimuacha Mariamu ambaye ni mchumba wake, Kamal alielewana sana na Teddy.

Yoyote katika familia kama alikuwa anahitaji kitu kwake na ana wasiwasi anaweza asikipate, atamwambia Teddy ili amuombee kwa niaba yake.

Teddy alisema au kuomba chochote kile kwa Kamal, kitatekelezwa hata kama siyo siku hiyo,




lakini tayari kitakuwa kwenye mpango wa kufanikishwa.

Wakati mwingine ikitokea hata Mariamu akikwaruzana na Kamal, humpigia mdogo wake na kumwambia kilichotokea, na yeye anaumaliza mzozo huo.

Kwa kifupi tu ni kwamba familia yote ilijua Kamal kwa Teddy hapindui. Wakawa wanasema kuwa damu zao zilipatana.

************************************

Akiwa kwenye chumba cha hoteli moja maeneo ya Ubungo, Kamal baada ya kuoga na kupata chakula cha usiku, alikaa kitandani na kumuwaza Mariamu. Akili ikaenda mbali sana, akakumbuka mara ya kwanza walipokutana kwenye Stendi Kuu ya Mabasi Msamvu na jinsi alivyomchezesha kindumbwendubwe.

Akakumbuka jinsi alivyokaa kwenye siti ya dirishani na kurejea, akamkuta msichana mrembo amekaa pale. Akakumbuka jinsi alivyomuamuru atoke, licha ya kwamba aliomba sana.

"Hapo ulipokaa ni kwangu. Nilikuwa nimekaa mimi awali. Nilishuka tu kwenda kupunga upepo nje."

"Okay, sawa kaka nimekuelewa. Ila naomba mimi nikae huku dirishani, wewe upande huu. Siti si hii hii moja bwana!"

"Kwa nini?"

"Samahani, ni kweli kuna kaka mmoja akaniambia hapo kuna mtu, lakini mimi naomba nikae huku dirishani kwa sababu huwa nina kichefuchefu."

"Okay, hata mimi nina kichefuchefu, ndiyo maana nimechagua siti ya dirishani. Kwanini na wewe hukuchagua siti ya dirishani?"

"Nilikuta zimejaa kaka yangu."

"Basi bahati mbaya sana. Naomba tu nikae kwenye nafasi yangu."

"Nakupisha kaka yangu." Akasema kwa sauti ya hasira kidogo iliyochanganyikana na aibu.

Ilikuwa ni mara ya kwanza Mariamu kukutana na mwanaume mgumu, kwani licha ya uzuri na urembo unaompa na kumsaidia kila kitu, lakini alikwama.

Kesi iliisha pale maeneo ya Bwawani gari ilipoharibika na kusimama. Ndipo walipopatana kwa namna ya ajabu kidogo.

Mariamu alikuja kugundua kuwa Kamal alifanya vile kwa ajili ya macho ya watu mle ndani ambao wangemuona dhaifu kwa wanawake na kumcheka.

"Dada siyo kama kuna kitu nataka, au naomba kutoka kwako, au nataka suluhu au kukuomba msamaha. Ila tu nataka nikuhakikishie kuwa nilichokifanya ndani ya basi hakikuwa kitu halisi!"

"Una maana gani ukisema siyo kitu halisi?"

"Nilipopanda basi abiria wote walioniona nimeshuka kabla basi halijaondoka pale Msamvu, walianza kunitazama sana, wengine walitabasamu, wengine wakacheka.

Mimi nikashangaa, hawa mbona wananiangalia sana wengine wakacheka? Kuna nini? Kufika kwenye siti yangu nakuona wewe. Kwa jinsi nilivyokutazama tu sura na ulivyo, nikajua sababu.

Unajua wewe ni msichana mrembo sana, Mungu kusema kweli amekujaalia, sasa nikagundua kuwa wale waliona nikifika pale na kukuta umekaa siti yangu nitanywea, nitakaa kwenye siti ile ile, lakini pembeni, siyo kule dirishani. Ndiyo kitu ambacho walikuwa wanasubiria, ndiyo maana nikafanya kitu kile."

**Dada siyo kama kuna kitu nataka, au naomba kutoka kwako, au nataka suluhu au kukuomba msamaha. Ila tu nataka nikuhakikishie kuwa nilichokifanya ndani ya basi hakikuwa kitu halisi!**

Mariamu alikubali kuamini kile alichoambiwa chini ya basi wakati linaendelea kutengenezwa, na kwa muda mfupi tu waliokuwa wakizungumza na kula, aligundua ni mwanaume mwenye huruma, upendo, kujali na mcheshi. Taratibu akaanza kumpenda. Kamal yeye alianza kumpenda mara tu alipomuona kwenye siti yake ya dirishani, licha ya kujishaua kote kule. Ndipo mapenzi yao yalipoanzia hadi uchumba.

Ghafla mawazo yakaondoka. Akajikuta yuko peke yake kwenye hoteli hiyo. Aliamua kuondoka katika hoteli ya Mwananyamala kwa Kopa ili kuwepa kufuatiliwa. Hakutaka kuishi hotelini kwa muda mrefu. Hata hapo alikuwa na mpango wa kukaa kwa siku tatu tu.

Aliachukua simu ya marehemu mchumba wake ambayo aliikuta siku ile alipokwenda nyumbani kwake na kutomkuta, kabla ya kupata taarifa ya kifo chake kesho yake, ikidaiwa amenguka akiwa anafanya mazoezi huko Tabata, lakini baadaye ndiyo ikasemana yeye ndiyo amemuua.

Akaanza kukagua meseji mbalimbali zilizokuwa zikitumwa. Alifanya hivyo ili kung'amua ambazo zingempa mwanga kuwa ni nani wanaweza kuwa nyuma ya tukio hilo.

Kati ya zote, akapata mechi tano ambazo zilionyesha za wanaume waliokuwa wanamtaka na kumfuatilia kwa muda mrefu.

Ndipo alipogundua kuwa Mariamu alikuwa mwanifu mno kwake, lakini meseji zote zilikuwa zinamtuhumu kwa kumpenda mtu kapuku, asiye na kitu ambaye ni yeye.

Ikaenda mbali sana, meseji zile zitaonyesha kuwa watu hao watamuua yeye, na baadaye kupata urahisi wa kubaki naye.

Lakini ipo meseji ambayo Mariamu aliwajibu kuwa kama wakimuua Kamal, wakitengemea ndiyo atawakubali basi wamenoa.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# AZIZ KI, FEI TOTO WAKIKWEPA KIATU CHA DHAHABU LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Stephane Aziz Ki wa Yanga na Feisal Salum wa Azam FC, wako kwenye vita kali ya kuwania ufungaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, wachezaji hao kila mmoja ameonekana kukwepa kuonekana anakihitaji kiatu cha dhahabu, badala yake kudai wanafunga mabao kwa sababu ya kuzisaidia timu zao.

Kabla ya mechi ya jana dhidi ya Tabora United, Aziz Ki alikuwa kinara kwenye ufungaji bora akiwa na mabao 17, na Fei Toto kabla ya mechi kati ya timu yake dhidi ya Kagera Sugar alikuwa nafasi ya pili kwa mabao 16, kila mmoja kwa wakati wake alionekana kutokuwa na hamu sana na ufungaji bora, ingawa walidai kama ikitokea basi watafurahia hilo.

Mara baada ya mechi dhidi ya JKT Tanzania, ambapo alifunga bao na kuiwezesha Azam kushinda mabao 2-0, mchezo uliopigwa Jumanne iliyopita, Uwanja wa Meja jenerali Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam, Fei Toto alisema anachofurahi ni kuiwezesha timu yake kushinda na si kufukuzana na mtu kwenye ufungaji bora.

"Mimi nafunga kwa ajili ya kuibeba timu yangu na wala sishindani na mtu au kuwaza tuzo la ufungaji bora, akili yangu kwa sasa ni kufunga kwa ajili ya kuisaka nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika, ila ikitokea huko mbele mabao yangu yakiwa mengi na kutofikiwa na mchezaji yoyote, nitafurahi pia," alisema mchezaji huyo aliyejiunga na kikosi hicho mwanzoni mwa msimu huu akitokea Yanga.

Jumatano iliyopita, Aziz Ki, alipachika mabao mawili, akiiongoza Yanga kuiadhibu Dodoma Jiji mabao 4-0, mechi ikichezwa, Uwanja wa Jamhuri Dodoma.

**Baada ya mechi hiyo, alisema ataendelea kufunga ili kuipatia timu yake ushindi na si kubeba kiatu cha dhahabu.**

"Tumepata ubingwa, lakini nitaendelea kufunga, sio kwa ajili ya kubeba kiatu cha ufungaji bora bali ni kuipa timu ushindi na kuwapa furaha mashabiki wa Yanga," alisema kiungo mshambuliaji huyo raia wa Burkina Faso.



Vijana wakiwania mpira wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## JKU yausogelea ubingwa Zanzibar

**Na Hawa Abdalla,** ZANZIBAR

MAMBO yameendelea kuwanyookea Maafande wa JKU SC katika harakati zao za mbio za ubingwa wa Ligi kuu ya Zanzibar kwa msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili Kocha wa timu hiyo, Salum Haji alisema kwa sasa jukumu kubwa anawaachia wachezaji kuhakikisha wanafanya vizuri katika michezo minne iliyobaki wakiwa uwanjani.

Alisema licha ya kubaki michezo michache lakini bado wanahitaji kushinda michezo yote ili kufanikiwa ndoto zao za kutwaa ubingwa msimu huu.

Alisema michezo iliyobaki ni migumu kutokana na ushindani uliopo kwa timu ambazo zinautaka ubingwa msimu huu.

Alisema kwasasa wachezaji wake wanapaswa kuzingatia zaidi nini timu hiyo inahitaji na kucheza kwa taadhari kubwa ili kuepuka majeruhi katika michezo hii michache ya kuumalizia msimu.

"Michezo hii ya mwisho kila mmoja ana nia ya kushinda ili kutimiza lengo lake, hivyo lazima wachezaji wachukue tahadhari kubwa kiuchezaji ili wajihepushe na kusababishiwa na majeraha,"alisema

Hata hivyo, alisema kuwa hakuna mchezo rahisi kati ya minne iliyobaki hivyo kila mchezo wanapaswa kuuchukulia umuhimu mkubwa ili kuepuka kupoteza.

## Ayoub akubali mwaka mmoja Simba

**Na Saada Akida**

GOLIKIPA wa Simba, Ayoub Lakred amefikia makubaliano ya kusalia ndani ya kikosi hicho kwa msimu ujao wa mashindano baada ya kusaini mkataba wa mwaka mmoja.

Imeelezwa kuwa baada ya mazungumzo kwenda vizuri pande zote mbili kati ya Simba na Kipa huyo atasaini mkataba wa mwaka mmoja kabla ya kuondoka kuelekea kwao kwenye mapumziko baada ya kumalizika kwa ligi.

Mtoa habari wetu alimelitonya Nipashe kwamba, Ayoub amekubali kusalia ndani ya timu ya Simba kwa msimu ujao

"Kulikuwa na mazungumzo na yameenda vizuri, Ayoub anasalia Simba kwa mkataba wa mwaka mmoja na atasaini kabla ya kuondoka kuelekea kwao kwa mapumziko baada ya kumalizika kwa msimu huu wa ligi," alisema mtoa habari huyo.

Nipashe lilimtafuta Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally ambaye alikiri kuwa kuna wachezaji wapo kwenye mazungumzo na wengine kuongeza mkataba kusalia ndani ya kikosi cha timu hiyo.

## Simba, Azam nje Ligi ya Vijana U 20

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za soka za vijana za Simba na Azam FC, zimetolewa kwenye hatua ya nusu fainali ya nane bora ya Ligi chini ya miaka 20, baada ya kupoteza mechi zao juzi.

Simba ilipokea kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Kagera Sugar ambayo imefanikiwa kutinga fainali, huku Azam ikiondolewa kwa mikwaju ya penalti 5-3 dhidi ya Dodoma Jiji, mechi zote zikipigwa, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Kwa matokeo hayo, fainali ya msimu huu ya Ligi ya Vijana chini ya miaka 20, itapigwa kati ya Dodoma Jiji dhidi ya Kagera Sugar.

Kocha wa Simba, Mohamed Mrishona, aliwapongeza wapinzani wao kwa kuwa bora katika mchezo huo, huku akisema makosa binafsi ya wachezaji wake ndiyo yaliyoamua mechi.

Kocha wa Kagera Sugar, Raymond Dotto alisema aliwasoma Simba katika michezo yao iliyopita na kugundua wana makosa wapi ambayo wameyatumia.

"Nashukuru hii ni ahadi niliyoiweka siku nyingi kutaka kuifikisha timu yangu hatua ya fainali, mechi ilikuwa ngumu, tumeshinda kwa sababu tumetumia makosa yao, niliwasoma nikagundua udhaifu wao uko wapi nikautumia," alisema kocha huyo.



Naye, Kocha wa Dodoma Jiji, Mohamed Muya (pichani), alisema waliingia kwa kuwaheshimu Azam na walijua ilikuwa ni mechi ya kutaka matokeo tu na si kingine na kweli wakaenda hadi kwenye mikwaju ya penalti na kushinda.

"Tuliwazidi Dodoma Jiji kwa kila kitu, lakini tatizo letu lilikuwa ni kuweka mpira wavuni tu, tukaja kuadhibiwa kwenye penalti," alisema Mohamed Badru, kocha wa timu ya Azam FC.

## ZISIKUPITE

### NEWCASTLE KUSAJILI WATATU

NEWCASTLE United inatumai kusajili wachezaji wawili wa kimataifa, huku mshambuliaji wa Everton, Dominic Calvert-Lewin, 27, na wa West Ham, Jarrod Bowen, 27, wakiwa kwenye rada yao. ***(Telegraph)***

### ISAK MILIONI 200

NEWCASTLE United wametakiwa kutoa pauni milioni 200 ili kumnunua mshambuliaji wa Sweden, Alexander Isak, 24, ambaye amekuwa akihusishwa na Arsenal. ***(Mirror)***

### TUCHEL KUMRITHI HAG

THOMAS Tuchel ambaye hana timu baada ya kuondoka Bayern Munich, ndiye mgombea anayeongoza kuchukua mikoba pale Manchester United ikiwa klabu hiyo ya Old Trafford itamfukuza Erik ten Hag baada ya fainali ya Kombe la FA. ***(Guardian)***

### MCKENNA YUPO TAYARI

KOCHA wa Ipswich Town, Kieran McKenna yuko tayari kuchukua mikoba ya Manchester United iwapo Erik Ten Hag ataondoka. ***(Manchester Evening News)***

### BRIGHTON YAJITOSA

KLABU ya Brighton ina uhakika wa kuipiku Chelsea kumwajiri Kieran McKenna lakini wanaweza kujaribu kumrejesha kocha wa zamani Graham Potter iwapo watashindwa kufanya hivyo. ***(Times)***

### MARESCA AWINDWA CHELSEA

CHELSEA ipo tayari kuomba Leicester City iliyopanda daraja iwaruhusu kuzungumza na Enzo Maresca kuhusu nafasi yao ya ukocha. ***(Sports)***

### STONES AFUATILIWA

KLABU ya Bayern Munich inamfuatilia beki wa England na Manchester City, John Stones, 29. ***(Football Insider)***

### ANALENGWA BAYERN

KIUNGO wa kati wa Manchester City na England, Jack Grealish, 28, analengwa na Bayern Munich. ***(Sun)***

### EDERSON HATAZUIWA

KLABU ya Manchester City haitamzuia mlinda lango wa Brazil, Ederson, 30, ikiwa mchezaji huyo anataka kuhamia Saudi Arabia. ***(90 Min)***

### BURNLEY YATAKA FIDIA

KLABU ya Burnley inataka fidia ya pauni milioni 17 kutoka kwa Bayern ili kumruhusu kocha Vincent Kompany kuchukua mikoba katika klabu hiyo ya Ujerumani. ***(Sky Sports Ujerumani)***

### SUMMERVILLE AWANIWA LIVER

LIVERPOOL imeelekeza mawazo yake kwa winga wa Leeds United, Crysencio Summerville, 22, baada ya kuamua kumnunua winga wa Newcastle United na England, Anthony Gordon, 23. ***(90 Min)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# POCHETTINO ATAJWA KUMRITHI SOUTHGATE

### Mwenyewe asema yupo tayari kubeba mikoba hiyo na kwamba...

**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino anaweza kuwa mshindani mkuu kuwa kocha ajaye wa England ikiwa Gareth Southgate atajiuzulu baada ya michuano ya Euro 2024.

**Southgate alikabidhiwa udhibiti wa timu ya taifa mwaka 2016, akichukua mikoba ya Sam Allardyce baada ya bosi huyo wa zamani wa West Ham kuondolewa kwenye wadhifa wake baada ya mechi moja tu ya kuiongoza.**

Tangu wakati huo, ameiongoza nchi hiyo kufika nusu fainali ya Kombe la Dunia mwaka 2018 na kutinga fainali ya Euro 2020. Lakini bado hajashinda taji akiwa na England na anaweza kuona Ubingwa wa Ulaya mwaka huu nchini Ujerumani kama fursa ya kufanya hivyo, akiwa na kizazi kipya cha dhahabu.

Hata hivyo, iwapo Southgate ataondoka baada ya Euro, gazeti la Daily Telegraph limeripoti kuwa Pochettino anaweza kuwa mstari wa mbele kubeba mikoba hiyo, huku kocha huyo wa zamani wa Chelsea akionekana kuwania nafasi hiyo.

Ilibainika Jumanne kwamba Pochettino aliachana na Chelsea baada ya msimu mmoja kuinoa The Blues.

Ilikuwa kampeni ngumu katika uwanja wa Stamford Bridge, huku kikosi kikijitahidi kuwa na uthabiti lakini kikiona mwanga wa matumaini kuelekea mwisho - kikipata ushindi mara tano mfululizo.

Kazi ya kuinoa England imekuwa ya kuvutia kwa muda mrefu kwa Pochettino, ambaye alionesha nia yake ya kwanza kumrithi Southgate baada ya Kombe la Dunia lililopita huko Qatar.

Akizungumza na The Athletic mwaka wa 2022, Muargentina huyo alikiri kwamba alikuwa "wazi kwa kila kitu" na alijisikia "raha" kusimamia England.

Pochettino alielezea hisia zake kuhusu soka la Uingereza msimu huu, ambapo alisema: "Tunapenda utamaduni wa Kiingereza na katika kila klabu, kama vile Southampton, kisha Tottenham.

"Mimi ni Muitaliano kupitia kwa babu yangu mkubwa. Alihamia Argentina, kisha nikahamia Hispania na kisha Ufaransa na kisha Uingereza. Na unaelewa sana unapoanza kuhama nchi jinsi watu wanavyokuchukulia.

"Lakini tulipokuwa Southampton, Tottenham na Chelsea, Waingereza wanatutendea vyema. Ni jambo la kushangaza. Sio sisi tu, familia zetu pia. Ndiyo maana ninahisi niko nyumbani ninapokuwa Uingereza."

Pochettino pia amekuwa akihusishwa na Manchester United ikiwa klabu hiyo itamfukuza kazi kwa shinikizo la kocha Erik ten Hag.

Southgate pia amehusishwa na kuhamia Old Trafford, ingawa mustakabali wa Ten Hag bado haujaamuliwa kwa sasa.

# RASHFORD: SITAONDOKA MAN UNITED



**MANCHESTER,** England

MARCUS Rashford hana nia ya kuondoka Manchester United baada ya kukosa nafasi kwenye kikosi cha England kuelekea michuano ya Euro 2024, hata kama kocha Erik ten Hag atasalia kuwa kocha wa klabu hiyo.

Rashford alikosekana kwenye kikosi cha kocha Gareth Southgate cha wachezaji 33 kwa ajili ya mechi ya majira ya kiangazi huko Ujerumani, kufuatia msimu ambao alifunga mabao nane pekee katika mechi 42 katika mashindano yote.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 alicheza nafasi ya nyota katika msimu wa kwanza wa Ten Hag huko Old Trafford, akifunga mabao 30 bora zaidi wakati United ikimaliza kungoja kwa miaka sita kwa taji kwa mafanikio katika Kombe la Carabao, lakini walijitahidi kudumisha kiwango chake. huku mashetani wekundu hao wakivumilia kampeni ya 2023/24 yenye matatizo.

United walimaliza katika nafasi ya nane kwenye Ligi Kuu England, wakikosa kabisa mashindano ya Ulaya ingawa kama wakiifunga Manchester City kwenye fainali ya Kombe la FA Jumamosi wanaweza kufuzu Ulaya, na Rashford hakuwa na uhakika wa kuanza kila mara mbele ya Alejandro Garnacho ambaye amekuwa akiimarika kila mara.

Rashford amekuwa akihusishwa na kuhamia kwa wapinzani wa Ligi Kuu Arsenal, na pia ni mchezaji anayevutiwa kwa muda mrefu na Paris Saint-Germain, ambaye alitafuta kuhamia mji mkuu wa Ufaransa kabla ya kusaini mkataba wa miaka mitano wa kuinoa United.

Lakini Rashford mwenyewe amesema bado anajitolea kwa United, na hisia hiyo haitabadilika ikiwa Mholanzi huyo ambaye hana presha ataendelea na jukumu lake kama kocha.

# Zirkzee kwenye rada za Arsenal



**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal inahusishwa na mpango wa kumsajili mshambuliaji kutoka nchini Uholanzi na Klabu ya Bologna ya Italia, Joshua Orobosa Zirkzee.

Siri ya mpango wa usajili wa mshambulaiji huyo mwenye umri wa miaka 23 imefichuliwa na Mwandishi wa Habari wa Sky Italia, Gianluca di Marzio, akiamini endapo usajili huo utafanikiwa, Arsenal watalamba dume.

Marzio amesema anafahamu kuwa Zirkzee yupo kwenye orodha ya wachezaji wanaopewa nafasi kubwa ya kusajiliwa huko Emirates Stadium kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu ya England na mMichuano ya kimataifa.

Hata hivyo, mwandishi huyo ameonesha wasiwasi kuwa huenda Zirkizee akapata changamoto ya kushindanishwa na washambuliaji wengine ambao watapendekezwa kusajiliwa klabuni hapo, katika kipindi hiki cha usajili wa majira ya Kiangazi.

Marzio amesema: "Kwa jinsi Arsenal wanavyocheza, nadhani Joshua Zirkzee anaweza kuwa msaada mkubwa kwao. Najua yuko kwenye orodha yao, lakini sijui kama yeye ndiye kipaumbele,"

"Pia yuko kwenye rada za Juventus na Milan, na kwa sasa yeye ndiye Mshambuliaji chipukizi anayefaa kwa wote."

"Lakini Zirkzee ana hali ya kushangaza katika mkataba wake, kwani Bayern wana chaguo la kumnunua tena kwa euro milioni 40, lakini ikiwa Bologna itamuuza kwa vilabu vingine, watapata asilimia 60 tu ya ada ya uhamisho."

"Inategemea kama Bayern wataamua kumnunua tena au la. Inategemea nani ataamua kumuuza Bayern au Bologna. Kwa hivyo ni hali ngumu katika suala hili."

# Toney ajipanga kuondoka Brentford

**LONDON,** England

IVAN Toney anaweza kuzingatia kuondoka kama mchezaji huru mwaka 2025 ikiwa atakosa klabu sahihi ya kujiunga nayo kipindi cha majira bya joto.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ambaye aliitwa kwenye kikosi cha awali cha wachezaji 33 cha England kwa Euro 2024 siku ya Jumanne, amebakiza miezi 12 katika mkataba wake wa sasa na yuko tayari kuihama klabu hiyo ili kuendeleza soka lake.

Toney aliwahi kuthaminiwa na kocha wa Brentford Thomas Frank kwa pauni milioni 100, huku raia huyo wa Denmark akisema Februari kwamba mali yake ya thamani 'ina uwezekano mkubwa kuuzwa msimu wa joto', lakini kwa muda mfupi sana uliosalia kwenye mkataba wake, Brentford itazingatia ofa zaidi ya pauni milioni 45.

Arsenal na Chelsea zinamuwania kwa muda mrefu Toney, huku Manchester United nayo ikitajwa kuwania saini yake.

Klabu zote tatu zinaelekeza macho yao kwa washambuliaji wengine wakuu, pia, huku Victor Osimhen, Benjamin Sesko, Viktor Gyokeres wakiwa miongoni mwa wanaohusishwa.

Toney yuko tayari kubaki na kusubiri kuondoka kama mchezaji huru baada ya kurejea Januari akitoka kifungo cha miezi nane kwa kukiuka kanuni za kamari.



# HABARI MICHEZO

## Yanga kutikisa

INATOKA UKURASA 24

Ali Kamwe alisema leo ni siku muhimu kwa Wananchi kushirikiana ubingwa wao na kuanza paredi ya Yanga na kombe litabebwa na Helkopta litazunguka jijini Dar es Salaam.

Mchezo mwingine utakaochezwa leo ni Azam FC dhidi ya Kagera Sugar.

## Mo Dewji

INATOKA UKURASA 24

itakuwa na kazi ya kuisaka nafasi ya pili kwa ajili ya kupata tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

Simba iliamua kuipeleka mechi hiyo jijini Arusha kwa sababu mbalimbali ikiwemo uhitaji wa mabao mengi, kwani mara ya mwisho ilipocheza kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha miaka minne iliyopita, iliichakaza Coastal Union mabao 7-0 katika mechi ya Ligi Kuu iliyochezwa, Novemba 21, 2020, yaliwekwa wavuni na John Bocco aliyefunga mabao matatu, 'hat-trick', mawili yakifungwa na Clatous Chama, Hassan Dilunga na Benard Morrison wakifunga bao moja kila mmoja.

Timu hiyo si tu inahitaji ushindi, bali pia idadi kubwa ya mabao kwani, haina uwiano mzuri wa mabao ya kufunga na kufungwa dhidi ya Azam ambayo nayo inalisaka nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa kwa udi ya uvumba, huku nayo ikishuka dimbani leo kucheza dhidi ya Kagera Sugar, Uwanja wa azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Simba na Azam zote zina pointi 63, zikiwa zimebakisha mechi mbili kila moja na mabao ya kufunga 56 kila timu, lakini, lakini Wanalambalamba wameruhusu mabao 20 wavuni, Wekundu wa Msimbazi wavu wao ukigushwa mara 25.

Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda amesema mechi ya leo ni muhimu, lakini akifurahia urejeo wa wachezaji Clatous Chama na Luis Miquissone.

"Tuna mchezo muhimu sana kesho, maandalizi kwa ajili ya mchezo huu yako tayari, tumekuja kutimiza tu kile ambacho tumekiandaa, naamini itakuwa mechi ngumu, yenye ushindani kutokana na mahitaji.

Mchezaji Pa Omri Jobe na Kibu Denis ndiyo watakosekama, lakini tunashukuru urejeo wa wachezaji, Luis Miquissone, Clatous Chama," alisema.Kocha Msaidizi wa KMC, John Matambala, amesema wapo tayari kuikabili Simba, ingawa alisema atawakosa Andrew Vicent 'Dante' na Ismail Gambo.

"Tuko tayari na mechi dhidi ya Simba, pamoja na uwanja kubadilishwa lakini sisi kama wanajeshi, tutacheza uwanja wowote kwa muda wowote.

Tunawakosa Dante na Gambo, ila Wibol Maseke atakuwepo," alisema Matambala.

# MWADUI KUITWA BIG MAN FC

Na Adam Fungamwango

SIKU moja tu baada ya kupanda Ligi cha Championship, timu ya Mwadui FC, imebadilishwa jina na sasa itajulikana kama Big Man FC.

**Makao makuu ya klabu hiyo ambayo awali yalikuwa mkoani Shinyanga, sasa yatakuwa Tanga.**

Akizungumza mjini Tanga, mmiliki mpya wa timu hiyo, Waziri Gao, amesema baada ya kuichukua, ameamua kuita jina hilo, ambalo ni lake mwenyewe la utani, huku akiahidi kutoa upinzani mkali msimu ujao kwenye Ligi ya Championship.

Gao, alisema kuwa ameichukua timu hiyo wakati timu hiyo ikijiandaa kucheza hatua ya nane bora ya Ligi Daraja la Pili, 'first league.'

"Nimeiita Big Man FC, ikiwa na maana mimi ni mtu mkubwa, unajua ndugu yangu, raha jipe mwenyewe na jina zuri jitafutie mwenyewe, mimi nimeona hili ndiyo zuri.

Nimeichukua wakati tunakwenda kucheza nane bora wa Ligi Daraja la Pili, tukaanza kuchezea huku Tanga, kusema kweli nimefarijika, mashabiki walikuwa wanajazana uwanjani na ngoma za mdumange wanashangilia, mpaka tukaingia hatua ya 'play off' na hatimaye tumepanda," alisema.

Alisema ameshaanza kujipanga kwa ajili ya kukiandaa kikosi chake, huku akionya kuwa ataleta upinzani mkali msimu ujao.

Mimi soka sijaanza leo, mimi ni mtu wa mpira siku nyingi na tayari nimeshaanza kupigiwa simu na baadhi ya wachezaji maarufu wakitaka kuja kuichezea timu hii kwenye Ligi ya Championship msimu ujao.

Kabla ya kubadilisha jina, timu hiyo ilifanikiwa kutinga hatua hiyo kwa ushindi wa mabao 5-2 dhidi ya Copco FC, ambapo katika mechi ya kwanza ilishinda mabao 3-0 na majuzi, ililazimisha sare ya mabao 2-2 na kuishusha Copco iliyotoka Championship.



Vijana wa Timu ya Eagle, Hashimu Ali kulia na Abeid Omary, wakiwania mpira wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika eneo la Mbande jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Tembo Warriors yasaka nafasi kombe la Dunia*

Na Saada Akida

BAADA ya kufungwa na Ghana katika hatua ya robo fainali ya Afrika (AAFCON), Kocha Mkuu wa Tembo Warriors, Salvatory Edward ameweka wazi kubadilisha malengo ya mashindano hayo na sasa anatafuta nafasi kwa ajili ya kucheza kombe la Dunia 2026.

Tembo Warriors walifungwa 4-1 na Ghana katika mchezo wa hatua ya robo fainali uliopigwa uwanja wa PetroSport, nchini Misri.

Tanzania leo inashuka dimbani tena dhidi ya mabingwa Angola kuendelea kuisaka nafasi adhimu ya kushiriki Kombe la dunia 2026 kuiwakilisha Tanzania na Afrika katika nafasi saba, zinazoenda kuiwakilisha kombe la Dunia.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Salvatory alisema mechi ya Ghana ilikuwa ya ushindani mkubwa, wachezaji walipambana lakini haikuwa bahati kwao.

Alisema licha ya kufungwa kwenye hatua ya robo fainali lakini bado wapo katika mashindano na wanajiandaa kwa mechi zijazo kutafuta nafasi ya kwenda kucheza kombe la Dunia.

"Malengo yetu yamebadilika baada ya kuhitaji kombe la Afrika, sasa tunahitaji kujipanga vizuri katika mechi zetu, mashindano magumu na tunapambana na matumaini yetu kuwa sehemu ya timu saba ambazo tutaenda kuiwakilisha nchi katika kombe la Dunia, 2026," alisema Salvatory.

Nahodha wa Tembo Warriors, Shadrack Hebron alisema wamepoteza mechi ya robo fainali na wana sahau matokeo hayo na kuweka nguvu zao kwenye mechi zijazo kutafuta nafasi ya kombe la Dunia.

"Bado hatujakata tamaa, tumepoteza mechi ya robo fainali lakini bado hatujaondolewa kwenye mashindano, sasa tunapambana kutafuta nafasi ya kufuzu na kwenda kucheza kombe la Dunia mwakani," alisema Shadrack.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo Dk. Suleiman Serera amewataka wachezaji na benchi la ufundi (Tembo Worriors) kuyachukulia matokeo waliyopata katika mechi yao dhidi ya timu ya Taifa ya Ghana.

"Tukiendelea kulia na kusikitika wala haitaturudishia kitu, tunachotakiwa kujua mwana michezo yeyote anayekuja kwenye mashindano anakuja kwa ajili ya kushinda, hakuna anayekuja kwa ajili ya kupoteza,"alisema

Aliwataka kutokuwa na simanzi bali waende kuboresha nafasi wanazozipata na kutumia katika mechi zingine, mechi za Afrika kipimo sahihi na kupambana kutafuta nafasi ya kufuzu kombe la Dunia.

Brigedia Generali Ismail Shajack Ismail mwakilishi wa Balozi wa Tanzania nchini Misri amewataka wachezaji na benchi la ufundi kwenda kujipanga vilivyo kupambania timu saba zitakazoshiriki Kombe la Dunia.

# Michezo

Jumamosi Mei 25, 2024

Nipashe




Rashford: Sitaondoka Man Utd UKURASA 22



Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), Patrice Motsepe (wa pili kushoto), akiwa ameongozana na, Rais wa mpira wa miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia (wa pili kulia), baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume mjini Zanzibar, kwa ajili ya kufunga mashindano ya African Schools Football Zanzibar jana. P**ICHA: JUMANNE JUMA**

# Yanga kutikisa Dar

**Na Saada Akida**

## Ni katika sherehe za kukabidhiwa kombe la Ligi Kuu huku...

TIMU ya Yanga leo inashuka dimbani kucheza na Tabora United katika uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam saa 10:00 alasiri, huku pia ikitarajiwa kukabidhiwa kombe lao la Ligi Kuu Tanzania Bara

**Sherehe za kukabidhiwa kombe hilo zitaanza majira ya saa 4:00 asubuhi kwa burudani mbalimbali kwenye uwanja huo kabla ya kuanza kwa mchezo huo .**

Timu hiyo inashuka dimbani ikiwa haina cha kupoteza, lakini itahitaji kulinda heshima yao ya kutopoteza mechi hiyo ambayo wanakabidhiwa kombe la ubingwa.

Muhimu kilichopo mbele yao ni kuona kiungo wao mshambuliaji, Stephane Aziz Ki anaendelea na kasi yake ya kufunga na kutoa pasi za mabao ili mwisho wa siku kuibuka mfungaji bora kwa idadi nyingi ya mabao ambayo kwa sasa amefung 17 na Feisal Salum wa Azam FC akiwa na mabao 16.

Kuelekea mchezo huo Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi alisema anahitaji kuona timu yake inacheza vizuri na kupata matokeo chanya na kufanikiwa kuvuna alama tatu muhimu katika mchezo wa leo.

Alisema mashabiki baada ya kumaliza mechi zote watapata muda wa kufurahia, lakini sasa wanaenda kutafuta matokeo chanya katika mchezo huo dhidi ya Tabora United.

"Mchezo huu ni muhimu kama michezo mingine licha ya kutwaa ubingwa, wachezaji wanatambua kuwa tunahitaji matokeo mbele ya Tabora United," alisema Miguel.

Mwakilishi wa wachezaji wa Yanga, Ibrahim Bacca alisema wamejiandaa vizuri na watapambana kutafuta matokeo mazuri na ushindi dhidi ya Tabora United.

"Hautakuwa mchezo rahisi lakini tumefanya maandalizi mazuri na tunahitaji kupata pointi baada ya ushindi wa leo ndio tutasheherekea ubingwa tulioupata pomoja na mashabiki wetu uwanja wa Benjamin Mkapa," alisema Bacca.

Kocha Msaidizi wa Tabora United, Benard Fabian alisema maandalizi yamekamilika ni mchezo muhimu kwao kutafuta matokeo ili kujiondoa kwenye nafasi ya chini ya msimamo.

Alisema hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu ubora wa wapinzani wao kila idara, wanaenda kucheza bila presha kwa sababu wanahitaji kupata matokeo ya kutafuta nafasi ya kubaki kwenye ligi kuu msimu ujao.

"Huu mchezo kwetu ni muhimu kutafuta alama muhimu, tutaingia kwa tahadhari kubwa katika mchezo huu kulingana na ubora wa Yanga, pia ni siku yao ya furaha ya kusherehekea Ubingwa. Tofauti na sisi tuna uhitaji mkubwa wa mchezo huu," alisema

Kwa mujibu wa Ofisa habari wa Yanga,

ENDELEA UKURASA 23

# Mo Dewji kusimamia mwenyewe usajili Simba

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikitarajiwa kushuka dimbani leo, Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha kucheza dhidi ya KMC, klabu ya Simba imesema mwekezaji wa klabu hiyo na Rais wa Heshima, Mohamed Dewji, atasimamia mwenyewe usajili wa wachezaji kwa msimu ujao wa mashindano.

Akizungumza jana jijini Arusha, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema baada ya manung'uniko na malalamiko mengi, sasa mwekezaji huyo ameamua kuingia mwenyewe katika harakati za usajili, huku akiwa na fungu kubwa la kutosha kwa ajili ya kupata wachezaji bora na wenye viwango vya juu msimu ujao.

"Fedha yote ya usajili ya msimu ujao atatoa Dewji, na mzigo ambao umetengwa kwa ajili ya usajili ni mkubwa.

Niwaambie, Mo tunaye sana na tunatamba naye, usajili huu unaokuja utausimamia mwenyewe kwa asilimia mia moja, kwa hiyo wanachama na mshabiki msiwe na wasiwasi, atasimama mwenyewe kwa miguu miwili kuhakikisha wachezaji bora na wa gharama wanatua kwenye klabu hii, mateso, manung'uniko, masononeko sasa basi," alisema Meneja Habari huyo.

Kwa misimu takriban mitatu, wanachama na mashabiki wa Simba wamekuwa wakilalamikia usajili, wakidai haifanywi kwa weledi, kwani wachezaji wanaoletwa hawakidhi viwango, wengi wao wakionekana hawana hadhi ya kuichezea klabu kubwa kama hiyo ambayo imekuwa ikicheza kwenye nafasi ya tano hadi saba kwa mujibu wa viwango vya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF).

Wakati huo huo, timu hiyo leo

ENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >